**UJENZI** wa Bwawa la Nyerere sasa wafikia asilimia 90

UKURASA 7



**ADAIWA** kujinyonga kisa kuelemewa na madeni ya vikoba

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Julai 13, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581370

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Dola ya Marekani yazidi kuadimika

UKURASA 2



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba

## Mbunge Silaa asema watu wanatumika kumpotosha Rais Samia



UKURASA 2

## Pinda ataka kuimarishwa kwa mfumo wa chakula

UKURASA 3



Waziri Mkuu Mstaafu na Mwenyekiti wa Baraza la kumshauri Rais kwenye masuala ya Kilimo na Chakula, Mizengo Pinda (wa pili kulia), akizindua mkakati wa miaka mitano wa kuimarisha masoko ya mazao jijini Dodoma jana. Anayemsaidia ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega na (wa pili kulia) ni Mwakilishi wa USAID, Plato Hieronimus. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

**MICHEZO** **AZAM YAANZA KUCHEZA ZA KIRAFIKI** UK. 23 **KATUNI** UK. 6



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, akifurahia na wanafunzi wa Shule ya Msingi Endiamtu, wilayani Simanjiro, baada ya kukagua miradi ya elimu na afya yenye thamani ya Sh. milioni 846 juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mbunge Silaa asema watu wanatumika kumpotosha Rais

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Ukonga, Jerry Silaa, ameibuka kuwajibu aliowaita wapotoshaji wa uendelezaji wa Bandari ya Dar es Salaam, akiwatahadharisha Watanzania kuwa kuna watu wanatumika kwa maslahi wanayoyajua ili kumwondoa Rais Samia Suluhu Hassan kwenye reli.

Silaa ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC), aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu sakata hilo.

Katika mkutano huo, Silaa alitaja sababu tano za kuitisha mkutano huo huku ajenda kubwa akiitaja kuwa ni yanayoendelea akisema, kuna watu wachache kwa sababu wanazozijua wanapotosha umma na Watanzania wenye nia njema wanayasikia na kutengeneza taharuki.

"Sababu yangu ya kwanza, mimi ni mwana- CCM ninayo ahadi kwamba, nitajielimisha kadri ya uwezo wangu na kutumia elimu yangu kwa faida ya wote.

"Nina wajibu pale ninapoona jambo linapotoshwa kutoa mtazamo ambao ninaamini ni sahihi. Pili, mimi ni Mbunge na jimbo langu wanahitaji majibu na mimi nina wajibu wa kutoa maelezo ya kuwapa majibu.

"Tatu, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati na jambo hili lilipita kwenye kamati na Katiba yetu inatoa nguvu kwa Bunge kuishauri na kuisimamia serikali. Nina wajibu wa kutoa ushauri wangu, lakini nina wajibu wa kusema na yale yaliyofanyika bungeni," alisema.

Silaa alitaja sababu ya nne ni suala la upotoshaji ambao alisema anaona umezidi kuwa mkubwa na Watanzania wanahitaji majibu na kwamba wajibu wake kujibu anayofahamu.

"Sababu ya tano ni kuwatahadharisha Watanzania, kuna watu wanatumika kwa maslahi wanayoyajua kwa jitihada kubwa za kumwondoa kwenye reli Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye wakati wote amekuwa akifanya kazi kubwa ya kujenga uchumi wa taifa na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi.

Katika maelezo yake, Silaa alidai wale wanaofoka, wanaopiga meza, anaamini kufanya hivyo kumebeba kile kilichopo nyuma yao kwamba, kuna msukumo mkubwa kuliko wanalolisema.

"Ukisikiliza wengi, mtu anaweza kuongea kwa dakika 15, lakini hakuna sehemu yoyote anafika kuzungumzia yale makubaliano. Zipo hoja za kisheria ambazo ninasikitishwa kwa baadhi ya wanasheria kuzijadili katika mrengo ambao hawafahamu ama wanafanya kwa makusudi.

"Hapa tulipofika mkataba, makubaliano inawezekana likawa ni swali limeulizwa sana na kujibiwa sana, mwisho wa siku itategemea huyo anayezungumza, anazungumza kwa nia njema ama kwa nia ovu.

"Anataka kujikita kwenye Kiingereza, anataka kujikita kwenye lugha ya sheria, kujikita kwenye tafsiri ya kiingereza kwenda Kiswahili rahisi, ama anataka kujikita kwenye lugha ya kiingereza cha sheria kwenda kwenye lugha ya kiswahili cha sheria.

"Mwisho wa siku ukitaka kujadili mambo yote hayo, makubaliano ambayo yameingiwa baina ya serikali ya Tanzania na serikali ya Dubai, ni mkataba ama makubaliano ambayo yanalenga kujenga msingi wa kisheria ya masuala yote yatakayoenda kuendeleza bandari.

"Utarudi pale pale, hii ni hatua ya kwanza, na zipo hatua nyingine ambazo watu hawataki kuzizungumza, wanajikita hapa mwanzo na kutengeneza hofu za kule mbele, ndiyo maana ninasema ni kwa sababu wanazozijua wao," alidai.

Kiongozi huyo alisema masuala yote ya forodha yataendelea kufanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na ya ulinzi na usalama yatabaki kwenye vyombo vya ulinzi na usalama.

Alisema usimamizi wa bandari utabaki palepale chini ya sheria sura ya 17 ya mwaka 2004 ambayo inatoa mamlaka ya usimamizi wa bandari zote kwa TPA.

Alidai watu wote wanaozungumza na kufoka, wamenunuliwa kwa sababu kwenye urasimu wote wapo wanaonufaika.

"Masuala yote ya mapato bandarini yataendelea kufanywa na TRA na yale ya ulinzi yatafanywa na vyombo vya ulinzi na usalama kwa sababu bandari ni mkoa wa kiusalama una vyombo vyote vya usalama na vitaendelea kufanya kazi," alisema Silaa.

Kuhusu kuchelewa kushusha mizigo bandarini alisema ni mzigo kwa nchi na yeye ni Mwenyekiti wa Kamati za Kudumu ya Bunge, "hata huko baadaye mtaambiwa Bandari mwaka huu imeendelea kuvunja rekodi ya makusanyo, lakini bado haitoshi. Mnaopita bararabani kule Barack Obama, mnaona meli zimepaki zinataka kushusha mzigo. Msidhani kusimama zinapenda, zinasubiri zamu ya kuingia nangani kushusha mzigo.

"Leo mfanyabiashara yeyote tunayemhudumia akiulizwa, anajibu anaweza kujua jinsi ya kufika bandarini, lakini hawezi kusema lini atashusha mzigo kwa sababu ya ucheleweshaji na wao kujikuta wakilipa milioni 60 hadi 90 ya ucheleweshaji huo na kuongeza gharama kubwa kwa walaji," alisema.

"Wiki iliyopita serikali iliingia mkataba na Uropean Union ya Budget Support, mliona watu wakijadili kuwa fedha hizi zinatoka kwa Mzungu? Lakini watu wameshika jambo moja tu, hivyo nashawishika kusema kuwa kuna nguvu inatumika nyuma ya hawa wanaopotosha. Ndiyo maana nimeona nije hapa kutoa wito kwa serikali juu ya suala hili la bandari," alisema.

# Dola ya Marekani yazidi kuadimika

**Na Mwandishi Wetu**

DOLA ya Kimarekani imeendelea kuadimika nchini na kuuzwa kwa gharama ya juu huku baadhi ya benki zikiiuza kwa masharti na nyingine zikisitisha kutoa huduma hiyo.

Baadhi ya benki hizo zimepunguza kiwango cha uuzaji wa fedha hiyo kwa mteja mmoja kwa siku kutoka Dola 2000 hadi 500 ili kuwahudumia wateja wengi kwa siku.

Mwandishi wa gazeti hili alitembelea benki na maduka yanayotoa huduma ya kuuza fedha za kigeni jijini Dar es Salaam na kukuta Dola ya Kimarekani ikiuzwa kwa Sh. 2,499 hadi Sh. 2,535 kutoka Sh. 2,410 hadi 2,015 mwezi uliopita huku ikinunuliwa kwa Sh. 2,420 hadi 2,440 kutoka 2,350.

Pia mwandishi alibaini kuwa baadhi ya benki hizo ikiwamo Tanzania Commercial Bank (TCB), Dar es Salaam Commercial Bank (DCB), Kenya Commercial Bank na Exim zimesitisha kuuza fedha hiyo, National Bank of Commerce (NBC) ikiuzia wateja wao pekee.

"Kama sio mteja wetu hatukuuzii dola dada, kwa sasa tunawahudumia wateja wetu tu kwa sababu upatikanaji wake umekuwa wa shida sana, jaribu kwenda hapo nje kuna duka wanatoa huduma hii watakusaidia," alisema mhudumu wa benki NBC.

Aidha, baadhi ya benki ikiwamo NMB na maduka yanayouza dola 500 pekee kwa mteja kwa siku huku CRDB na Akiba Commercial Bank ikiuza dola 1,000 na wateja wanaohitaji zaidi ya hapo wanatakiwa kuomba siku tatu hadi wiki kabla.

"Mteja anayetaka dola 1000 hadi 1,900 akishaweka oda tunakwenda kutoa taarifa kwa meneja wa matawi, ili atupe ruhusa ya kumpa na wale wanaotaka zaidi ya 2,000 inabidi tuombe kibali cha kumpa kutoka idara ya fedha za kigeni," alisema mfanyakazi wa Akiba Commercial ambaye hakutaka jina lake liandikwe.

Mfanyabiashara wa nguo za watoto Kariakoo, Dennis James, alisema kadili upatikanaji wa fedha hiyo unavyokuwa mgumu biashara yake inazidi kudhorota kwa sababu uagizaji wa mzigo kutoka nje unategemea zaidi fedha hizo.

"Hali ni ngumu sana, ili upate kiasi cha dola unachohitaji inabidi utembee maduka yote ya hapa jijini kwa sababu sasa hivi wanauza dola 500 hadi 1,000 tu, na unakuta ninahitaji dola 20,000 nikalipie mzigo," alisema Dennis.

Aliiomba serikali na BoT ziingilie kati ili wawe wanalipia mizigo kwa pesa ya nchi wanayochukua bidhaa kwa kipindi hiki ambacho upatikanaji wa dola umekuwa wa shida.

"Kwa sisi tunaochukua mizigo China tuwe tunalipia fedha ya nchi hiyo kwa sababu upatikanaji wake hauna shida, hii itauondolea usumbufu na kufanya biashara zetu zishamiri kama zamani, kwa kweli uhaba wa dola unaumiza sana biashara," alilalamika.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Wizara ya Fedha, Benny Mwaipaja, alisema hawahusiki na jambo hilo na kumwelekeza mwandishi awasiliane na BoT.

Akizungumza na wahariri wa vyombo vya habari wakati wa semina kuhusu mwenendo wa uchumi nchini Juni 6, mwaka huu, Mkurugenzi wa Tafiti na Sera za Uchumi wa Benki ya Dunia, Dk. Suleiman Missago, alisema Tanzania ina uhumilivu wa upatikanaji wa dola licha ya ukwasi wake kuathirika duniani.

Alisema BoT bado ina akiba ya fedha za kigeni ikilinganisha na nchi nyingine lakini inatumika kwa uangalifu kutokana na hali ya upatikanaji wake kuendelea kuwa mbaya ulimwenguni kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo vita ya Urusi na Ukraine ambayo haijulikaani itaisha lini. "Sisi hatupo katika crisis (mgogoro), tuna upungufu. Na kutokana na uhimilivu huo ndiyo maana kila siku tunauza dola milioni mbili kwa benki ili isaidie kile ambacho kipo kule. Upungufu siyo kwamba zimeisha, unaposema kuna upungufu wa dola huko sokoni unaweza kuwa sahihi, lakini siyo uje ukaaminisha watu kwamba hazipo," alisema.



Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini, Priscus Tarimo (wa pili kushoto), akipata maelezo kuhusu uzalishaji wa vinywaji baridi hasa maji ya kunywa ya Kilimanjaro kutoka kwa mmoja wa wafanyakazi wa kiwanda cha vinywaji cha Bonite Bottlers, mjini Moshi mkoani Kilimanjaro hivi karibuni. **PICHA: JAMES LANKA**

# Pinda ataka kuimarishwa mfumo wa chakula

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amesema umaskini uliopo unatokana na kutoweka vizuri mfumo wa chakula ambao unaisababishia serikali gharama kubwa kukabiliana na utapiamlo na kutibu magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Pinda ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Kumshauri Rais kuhusu masuala ya Kilimo na Chakula, alitoa kauli hiyo jana kwenye uzinduzi wa Mpango Mkakati wa kuendeleza kilimo kwa mwaka 2023 hadi 2027 jijini hapa unaolenga kuinua uchumi katika sekta ya kilimo.

Alisema takwimu zinaonesha hali ya umaskini na kutaka watembelee vijijini kufanya utafiti na watakaporejea wajiulize nini kifanyike ili kuondokana hali hiyo.

"Ukitembelea vijijini ndiyo utajua kama bado tuna hali ya chini ya umaskini, hivyo jitihada zinapaswa kuwekwa ili kuhakikisha wakulima wanapata elimu ya matumizi ya ardhi ikiwamo kujua ni mazao gani yanapaswa kulimwa kwa ajili ya kuweka mfumo mzuri wa chakula kwa jamii."

"Tulivyokaa hapa hatuwezi kulijua jambo hii jamii hatuwezi kujua umaskini ulivyo, lakini nenda vijijini ukirudi ujiulize ulichokiona hali ya umaskini kwa taifa letu bado iko chini, pamoja na mengine yote ambayo tunafanya vizuri," alisema.

Alisema kama taifa limefanikiwa kuondoa ujinga katika elimu hakuna sababu ya kushindwa kuondoa umaskini kwa kuweka mfumo wa chakula vizuri na kusaidia jamii kula chakula kinachostahili.

Alisema Taasisi ya Kuendeleza Kilimo Afrika (AGRA) imekuja na Mpango Mkakati wa kuendeleza sekta ya kilimo kusaidia taifa, ili kufanya vizuri katika suala la uzalishaji wa chakula. Aliiomba AGRA kujikita katika uwekezaji wa kilimo cha umwagiliaji, ili kulisaidia taifa kuingia kwenye ushindani na mataifa makubwa kwa upande wa kilimo, kwa sababu ardhi ipo pamoja na vyanzo vya maji.

Pamoja na hayo, aliitaka Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na viwanda wafanye kazi pamoja ili kuondoa umaskini na kufikia asilimia 10 kwenye kilimo ifikapo 2030.

Naye Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema serikali itaendelea kushirikiana na AGRA kwa ajili ya kutekeleza mpango mkakati huo ili kuhakikisha taifa linazidi kuinuka kiuchumi. Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweri, alisema wizara imetenga Sh. milioni 800 kwa ajili ya kuwapa wajasiriamali kwa kutafsiri masoko

kwa njia ya uhalisia huku akisisitiza hadi sasa wamesajili wakulima milioni 3.3 na kuwapatia mbolea ya ruzuku.

Meneja wa AGRA nchini, Vianey Rweyendela, alisema bajeti ya utekelezaji wa mkakati huo imeongezeka ambao utagharimu Sh. trilioni 1.2.

# Adaiwa kujiua kisa deni la vikoba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VERONICA Petro (45) anadaiwa kujiua kwa kunywa sumu ya dawa ya kuulia wadudu kisa deni la vikoba analodaiwa.

Ndugu wa marehemu, Maria Petro akizungumza na Nipashe, alisema kabla ya kifo chake, aliwapa taarifa kuwa anadaiwa deni kubwa la fedha bila kutaja kiasi baada ya kukopa katika vikundi tofauti.

Mdogo huyo wa marehemu alisema dada yake alishawatamkia kuwa kutokana na deni analodaiwa, atachukua uamuzi wa kujiua lakini walijua kuwa anatania.

"Kweli alishatutamkia kuwa ana madeni na atachukua uamuzi wa kujiua maana hana uwezo wa kulipa. Tulijia anatania kuwa hatachukua uamuzi huo maana tuliona ni mtu mzima mwenye akili timamu," alisema.

Alisema majira ya saa 6:00 mchana, Julai 2, mwaka huu, kabla ya kufikwa na mauti, alifika kwa mjomba yao eneo la Jang'ombe, mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja na kukutana na mtoto wa mjomba wao na kuendeleza usemi wake kwamba kero ya deni lake kuwa lishakuwa kubwa, hivyo atachukua uamuzi wa kujiua.

"Yule mdogo wetu mtoto wa mjomba alimsihi sana na kumwambia usichukue uamuzi huo lakini baada ya mazungumzo hayo muda si mrefu alikwenda chooni kwa ajili ya kujisaidia na kwenda kujipumzisha uani katika nyumba ya mjomba.

Ghafla akasikia kishindo kumbe kishaanguka na povu mdomoni linamtoka chini kukiwa na kichupa cha dawa, yaani sumu," alisema.

Pia alisema Veronica alikuwa ni mjane lakini ana watoto wawili na alikuwa mjasiriamali (mama lishe) akiuza chapati katika eneo la Mkunazini, Mjini Unguja.

Hata hivyo, alisema baada ya kifo cha dada yao, watu mbalimbali wanajitokeza kuja kudai fedha zao.

"Kwa kweli deni kamili analodaiwa hatulijui na wala mwenyewe hakuwahi kusema ni kiasi gani. Lakini baada ya kufikwa na mauti, watu mbalimbali wanajitokeza kuja nyumbani kudai madeni.

Wako waliofika wanasema wanadai Sh. milioni moja," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Richard Mchovu, alikiri kutokea kwa tukio hilo na kuthibitisha kuwa chanzo cha mama huyo kujiua ni madeni aliyokopa katika vikoba.

Alisema uchunguzi wa suala hilo unaendelea ili kujua ni sumu ya aina gani aliyokunywa hivyo kumsababishia kifo.

Kutokana na tukio hilo, Kamanda Mchomvu aliwataka wananchi kuridhika na kipato walichonacho na kutokopa fedha kupitiliza bila kuwa na uwezo wa kurejesha na matokeo yake kupata msongo wa mawazo na hatimaye kujiua.

"Kujiua si suluhisho tafuta watu wakusaidie ili kulipa deni kuliko kujichukulia hatua mikononi,' alisema Mchomvu. Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Hospitali ya Mnazi Mmoja, Ali Azizi Masoud, alikiri kupokea mwili wa marehemu huyo uliofikishwa hospitalini hapo Julai 2, mwaka huu.

Alisema mwili wa marehemu ulishakabidhiwa kwa ndugu zake na kuzikwa katika makaburi ya Mwanakwerekwe, Mjini Unguja, Julai 4, mwaka huu.

# TCRA CCC yaipa tano serikali kuondoa tozo miamala kidijitali

**Na Jenifer Gilla**

BARAZA la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano Tanzania (TCRA CCC), limeipongeza serikali kwa kuondoa tozo kwenye huduma ya kutuma miamala ya fedha kidijitali.

Vilevile, limeipongeza kwa uzinduzi wa mradi wa ujenzi wa minara mipya 758 katika kata 713 Tanzania Bara na 48 katika shehia 38 Zanzibar na kuongeza uwezo na nguvu ya minara 304 katika maeneo mbalimbali nchini.

Limesema kuondolewa kwa tozo hiyo kunachochea ukuaji wa matumizi ya fedha kidijitali na kuimarisha usalama wa fedha za watumiaji hususani kupitia simu za mkononi na kuongeza ushiriki wa Watanzania katika mfumo jumuishi wa fedha.

Rais Samia alikubali ombi la Wizara ya Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Nape Nnauye, kufuta tozo za miamala za kutuma pesa kwa simu za mkononi mapema mwezi huu na kwamba sasa watumiaji wanatozwa wanapofanya miamala ya kutoa fedha kwa wakala.

Taarifa iliyotolewa na baraza hilo juzi, ilieleza kupungua kwa tozo hiyo pia kutachochea matumizi ya fedha kidijitali ambayo hurahisisha malipo mbalimbali, kuongeza uwazi, kuweka kumbukumbu za malipo na usalama wa fedha za watumiaji.

"Baraza linatambua kwamba mfumo imara na salama wa malipo na miundombinu ya kidijitali ni mojawapo ya nguzo kuu za uchumi wa kidijitali Tanzania ambavyo ni vipaumbele vya serikali katika sekta ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na katika kuimarisha ustawi wa Watanzania," ilieleza taarifa hiyo.

Aidha, ilisema kukamilika kwa minara hiyo kutawezesha watumiaji wa simu za mkononi maeneo ya vijijini kupata huduma za intaneti ya kasi na kuongeza wigo wa watumiaji wa huduma za mawasiliano kunufaika na kushiriki katika mapinduzi ya uchumi wa kidijitali.

Baraza hilo lilitoa wito kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano, hasa za fedha kupitia simu za mkononi na mifumo ya kidijitali, kutumia fursa hii ya kuondolewa kwa baadhi ya tozo kufanya miamala kwa uhakika na ufanisi zaidi kwa shughuli zao za kiuchumi, kijamii na kibinafsi.

Vilevile, limewataka watumiaji hao kujihadhari na wahalifu kwa kulinda namba za siri wanapotumia mitandao hiyo kufanya miamala ya kifedha au huduma nyingine na kutoa taarifa kupitia namba 15040 pindi wanapopata ujumbe wowote wenye kiashiria cha utapeli.

Aidha, limewasihi Watanzania kulinda miundombinu ya mawasiliano ili iwahudumie kwa muda mrefu na kuunga mkono jitihada za serikali kuifanya Tanzania kuwa ya kidijitali.

# Mtoto adaiwa kujinyonga, familia yafunguka

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MAPYA yameibuka katika sakata la mwanafunzi wa darasa la tano, Alex Salehe (11) wa Shule ya Msingi ya Mchepuo wa Kiingereza ya Mother Kevin Integrated English Medium iliyoko Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, baada ya baba yake mzazi kudai kilichosababisha mwanawe kujinyonga ni michezo ya kuigiza.

Alex alipoteza maisha Julai 5, mwaka huu, majira ya alasiri akiwa nyumbani kwao kitongoji cha Majengo, Kata ya Stesheni.

Inadaiwa kuwa, mwanafunzi huyo alijinyonga kwa kutumia nguo kwenye miundombinu ya kuanikia nguo iliyojengwa pembezoni mwa nyumba yao.

Akizungumzia mkasa huo, baba mzazi wa mwanafunzi huyo, Salehe Mgonja alisema: "Nahisi ilikuwa michezo tu ya watoto. Hapo alipokutwa na mauti. Nilikuwa nimejenga miundombinu ya kuanika nguo baada ya kumaliza kufuliwa. Mimi naamini kabisa hiyo ni michezo."

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi, Simon Maigwa, alisema kwamba mtoto huyo anadaiwa alijinyonga wakati anacheza na msaidizi wa ndani (jina limehifadhiwa), aligundua hilo baada ya dakika 10.

"Polisi inachunguza. Tunafanya ufuatiliaji ili tujiridhishe kuhusu taarifa hizi kulingana na umri wake. Mashaka yetu ni umri wake, lakini niseme uchunguzi unaendelea ili tuweze kujiridhisha pamoja na kwamba tumepata taarifa za awali ila tunataka tupate kwa pande zote mbili, kama kweli hayo yalifanyika.

"Mtu ambaye angeweza kutupa usahihi ametangulia mbele za haki. Nachoweza kuthibitisha kwa sasa hilo tukio la kujinyonga lipo na tunaendelea na ufuatiliaji, lakini ni kifo cha kawaida," alisema Kamanda.

Mkuu wa Watawa wa Shirika la Dada Wadogo wa Mtakatifu Fransco Tanzania na Msimamizi wa Taasisi ya Elimu ya Mother Kevin Integrated, Bridget Kokiambo alisema, "kilichotokea siku ya Jumatano ya Julai 5, 2023, mtoto Alex hakufika shuleni na wala hakuwa na tatizo lolote linalohusu malipo ya ada, wala usafiri wa gari la shule. Lakini majira ya saa 10 jioni, tulipokea taarifa za mshtuko sana, kwamba mtoto Alex amefariki dunia.

"Sisi kama Taasisi ya Mother Kevin, hatujui kabisa kilichotokea. Tunasikia tu na tunashangaa kuhusu hizo taarifa zinazozagaa zinatoka wapi.

"Tunaomba mamlaka husika zichunguze, kwa sababu hayo yanayozungumzwa huko ni kumtia mzazi msongo wa mawazo. Mzazi ambaye amepoteza mtoto angetarajia jamii imtulize, impe pole kwa kumpoteza mtoto.

"Sisi pia ni walezi na jamii ilipaswa itupe pole kama taasisi kwa kumpoteza mtoto, lakini kinyume chake, jina la shule linachafuliwa na kutuharibia mshikamano wa pamoja tulionao na huyo mzazi," alisema Mtawa Bridget.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya ya Same na Msimamizi wa Kitengo cha Familia na Watoto, Alli Shehoza, alisema kitengo hicho kinaendelea kufanya uchunguzi wa kijamii kuona taarifa za mtoto zilikuwaje na kuendelea kutoa msaada wa kisaikolojia kwa familia, shule na wanafunzi wa shule hiyo.

"Kwa kweli tunaendelea kufanya kazi na shule kuelimisha watoto, kuelimisha wazazi na walimu ni namna gani wanaweza kuwaelimisha na kuwa karibu na wanafunzi.

"Tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha mtoto aliyedaiwa kujinyonga katika wilaya yetu. Tukio hili limenishangaza, ni tukio ambalo linasikitisha hasa ukizingatia hatuna matukio ya namna hiyo Same.



Ofisa Mazingira wa Bodi ya Bonde la Wami/Ruvu Ofisi ya Mkoa wa Dar es Salaam, Hhau Sarwart (katikati), akipanda mti mita 60 kutoka Mto Kizinga, wilayani Temeke jana, lengo ikiwa ni mwendelezo wa kampeni ya utunzaji wa vyanzo vya maji mkoani humo. Bodi hiyo, imepanda miti 2,000 katika chanzo hicho kinachotumika na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kuhudumia wakazi wa wilaya hiyo. **PICHA: FRANK MONYO**

# Barrick yailipa serikali bilioni 340/-

**Na Faustine Feliciane, aliyekuwa** MARA

SERIKALI imesema imeshapokea Dola za Marekani milioni 140 (zaidi ya Sh. bilioni 340) kutoka kwa kampuni ya uchimbaji dhahabu ya Barrick ikiwa ni makubaliano waliyoingia na serikali ya awamu ya tano chini ya hayati John Magufuli.

Katika makubaliano ya mapitio ya mkataba wa kampuni hiyo na serikali, Barrick watatoa Dola bilioni 300 na fedha ambazo imepata ni sehemu ya fedha hizo.

Akizungumza katika mkutano wa viongozi wa kampuni hiyo, serikali ya mkoa na Wizara ya Madini, Naibu Waziri wa wizara hiyo, Steven Kiruswa, aliwashukuru Barrick kwa kuendelea kutekeleza makubaliano ya mkataba huo.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wawekezaji ambao wanafuata na kusimamia makubaliano waliyoingia.

"Serikali tunaendelea kunufaika na makubaliano mapya na kampuni hii ya Barrick, hii yote ni kuhakikisha rasilimali za nchi zinanufaisha taifa letu," alisema Kiruswa. Aidha, Mkurugenzi wa Uwekezaji wa ndani kutoka ofisi ya hazina, Lightenes Mauki, alisema pia kwa mwaka wa fedha ulioisha Juni 31, mwaka huu, serikali pia imepokea gawio la Dola za Marekani milioni 36 kati ya Dola milioni 52 wanazotakiwa kupata kutokana na ushirikiano wa kampuni hiyo na kampuni ya Serikali ya Twiga Mineral Cooperation.

"Tunafahamu pesa zilizobaki za gawio zipo kwenye mchakato wa kulipwa," alisema Mauki.

Mkurugenzi Mkuu na Rais wa Barrick, Dk. Mark Bristow, alisema mbali na kulipa pesa hizo, kampuni hiyo itaendelea kusaidiana na serikali katika kutatua changamoto zinazowakabili wananchi wanaoishi maeneo yanayozunguka migodi yao.

Alisema wameahidi kusaidia na wataendelea kufanya hivyo katika maeneo mbalimbali kwenye sekta za elimu, afya na miundombinu.

Oktoba mwaka 2017, serikali na Barrick ziliafikiana kuwa kampuni hiyo kuilipa Serikali ya Tanzania hisa ya asilimia 16 na mgawo wa asilimia 50 ya mapato ya mauzo ya dhahabu kutoka migodi inayoimiliki.

Barrick pia walikubali kutoa Dola za Kimarekani milioni 300 kama malipo ya kuonesha nia njema ya kufidia fedha zilizotokana na upotevu wa mapato kutokana na biashara ya kampuni hiyo.

Wakati huo huo, kampuni hiyo imetenga Sh. bilioni 97 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kahama-Kakora yenye urefu wa kilometa 137.9.

Rais na Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Dk. Mark Bristow, alisema usanifu umeshafanyika na wametangaza zabuni ili kumpata mkandarasi atakayejenga barabara hiyo.

"Tuliahidi kujenga barabara ya Kahama-Kakora, niwathibitishie hapa, ujenzi utaanza hivi karibuni baada ya kumpata mkandarasi, fedha tumeshazitenga," alisema Bristow. Pia, Barrick inatambua umuhimu wa barabara hiyo ambayo itafungua fursa za kiuchumi kwa wananchi wa maeneo hayo ambao watakuwa na uhakika wa kusafirisha bidhaa zao mbalimbali kutoka Kakora kwenda Kahama.

# Ndejembi ataka maeneo ujenzi shule yetengwe kukidhi mahitaji

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Deogratius Ndejembi, amesema kuna umuhimu wa kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa shule ili kukidhi mahitaji yanayotokana yakiwamo ongezeko la wanafunzi pamoja na kutatua kero ya kutembea umbali mrefu.

Ndejembi alitoa wito huo juzi mkoani Dar es Salaam, wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya elimu inayojengwa kupitia miradi ya BOOST na SEQUIP katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Kinondoni.

Alisema maeneo hayo yakitengwa, kuna ulazima wa kujenga shule za ghorofa badala ya majengo ya chini ili kutatua changamoto ya kukosa viwanja vya michezo vya watoto ambavyo ni muhimu kwa ajili ya kujenga afya ya akili.

"Michezo ni muhimu kwa ajili ya afya ya akili na makuzi ya watoto, hivyo ni lazima kuwapo ushirikiano wa viongozi kuanzia ngazi ya mtaa, kata, halmashauri, wilaya na mkoa katika kuhakikisha shule zinajengwa kwenda juu ili kupata maeneo ya viwanja vya michezo," alisisitiza Ndejembi.

Kwa mujibu wa Ndejembi, serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuboresha elimu ya msingi na sekondari, hivyo ni lazima kuendelea kutenga maeneo ya ujenzi na kuyatumia vizuri ili yawe na tija.

Aidha, Ndejembi aliipongeza Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Manispaa ya Kinondoni kwa kukamilisha ujenzi wa shule mpya na ukarabati wa miundombinu ya elimu, kupitia fedha za miradi ya BOOST na SEQUIP zilizopatikana kutokana na jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amedhamiria kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, alimshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha za ujenzi wa miundombinu ya elimu kupitia BOOST na SEQUIP na kuahidi kuendelea kusimamia vizuri matumizi ya fedha hizo ili ziwe na manufaa kwa taifa.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## TANGAZO KWA WAGUSWA WA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP)

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika ya Mashariki (EACOP) ni njia ya bomba itakayosafirisha mafuta ghafi yatakayozalishwa kutoka viunga vya mafuta vya Ziwa Albert nchini Uganda mpaka bandari ya Tanga, nchini Tanzania ambapo mafuta baadae yatasafirishwa na kwenda kuuzwa kwenye masoko ya kimataifa. Bomba litafukiwa chini na litatandazwa urefu wa kilometa 1,443 kuanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Rasi ya Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania, ambapo asilimia 80 ya urefu wa bomba ipo nchini Tanzania.

Mradi unawatangazia Waguswa wote ambao hawajaonyeshwa stahiki za fidia zao pamoja na kusaini mikataba ya malipo ya fidia wajitokeze haraka iwezekanavyo ili waweze kukamilisha zoezi hili. Waguswa wafuatao wanaombwa kuwasiliana na Mradi.

**MKOA WA KAGERA**

| Jina | Wilaya | Kijiji | Kata |
|---|---|---|---|
| Jonasan Mugisha Rwiza | Bukoba DC | Kyaitoke | Kyaitoke |
| Murishidi Hausi Murishid | Bukoba DC | Kobunshwi | Mugajwale |
| Respidius Daniel Binamungu | Bukoba DC | Rwigembe | Ngenge |
| Zainabu Abdallah Gabo | Muleba | Rwigembe | Ngenge |
| Eliud Anatory Mapinduzi | Muleba | Nyakanyasi | Ngenge |
| Bideston John Rwashegeza | Muleba | Kiguzi | Karambi |
| Nila Bukarashi Ng'Huba | Biharamulo | Kasozikabaya | Nyamigogo |

Kwa mawasiliano zaidi piga simu kwa **Mratibu wa Mahusiano ya Jamii wa Mradi [Adolf Ndunguye, 0744197768, Charles Shagi, 0699807077]**

**MKOA WA MANYARA**

| Jina | Wilaya | Kijiji | Kata |
|---|---|---|---|
| Deogratius Goranga Hilonga | Hanang | Masusu | Gisambalang |
| Gideon Gasper Mbwelwa | Kiteto | Ndorokoni | Njoro |
| Jackson Nonya Nhangala | Kiteto | Kimana | Partimbo |
| Matata Juma Nyange | Kiteto | Kimana | Partimbo |
| Michael Ammy | Hanang | Masusu | Gisambalang |
| Salum Ramadhan Mazila | Kiteto | Amei | Loolera |
| Twahibu Abdallah Wisu | Kiteto | Olpopong' | Njoro |

Kwa mawasiliano zaidi piga simu kwa **Mratibu wa Mahusiano ya Jamii wa Mradi [Emil Msisiri, 0742267636, Laurence Sigalla, 0699807053]**

Waguswa wa Mradi waliotajwa, wanaombwa kuwasiliana na Mradi wa EACOP ili waweze kuonyeshwa stahiki zao, kutia sahihi mkataba wa fidia ili malipo ya fidia yaweze kuendelea kufanyika. Waguswa wanaweza kuwasiliana na Mradi wa EACOP kupitia:

- Kupiga Simu namba ya bure [0800780068]
- Kuandika barua pepe [info.tz@eacop.com]
- Wasiliana na Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa

Waguswa wa Mradi ni lazima wawe na nyaraka muhimu ambazo ni fomu za uthamini walizopewa wakati wa zoezi la uthamini pamoja na vitambulisho. Nyaraka zitakaguliwa na timu ya Mradi kuhakiki usahihi wa utambulisho wao na kuthibitisha kama kweli ni waguswa wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki,
**Waguswa wanaombwa kuwasiliana na Mradi wa EACOP haraka iwezekanavyo.**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## TANGAZO KWA WAGUSWA WA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP)

Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika ya Mashariki (EACOP) ni njia ya bomba itakayosafirisha mafuta ghafi yatakayozalishwa kutoka viunga vya mafuta vya Ziwa Albert nchini Uganda mpaka bandari ya Tanga, nchini Tanzania ambapo mafuta baadae yatasafirishwa na kwenda kuuzwa kwenye masoko ya kimataifa. Bomba litafukiwa chini na litatandazwa urefu wa kilometa 1,443 kuanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Rasi ya Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania, ambapo asilimia 80 ya urefu wa bomba ipo nchini Tanzania.

Mradi unawatangazia Waguswa wote ambao hawajaonyeshwa stahiki za fidia zao pamoja na kusaini mikataba ya malipo ya fidia wajitokeze haraka iwezekanavyo ili waweze kukamilisha zoezi hili. Waguswa wafuatao wanaombwa kuwasiliana na Mradi.

**MKOA WA GEITA**

| Jina | Wilaya | Kijiji | Kata |
|---|---|---|---|
| Baslides Zege Nyanda | Mbogwe | Shinyanga B | Nyakafulu |
| Richard Dutu Mashindike | Chato | Nyambiti | Nyamirembe |
| Rebeka Leonard Dida | Chato | Ilelema | Iparamasa |
| Happnes John Ndabakenga | Mbogwe | Shinyanga B | Nyakafulu |

Kwa mawasiliano zaidi piga simu kwa **Mratibu wa Mahusiano ya Jamii wa Mradi [Mathew Kihulya, 0742256433, Theophil Celestine, 0628706338]**

**MKOA WA SHINYANGA**

| Jina | Wilaya | Kijiji | Kata |
|---|---|---|---|
| Hangwa Embasi Manyilizu | Kahama | Seeke | Zongomera |
| Elizabeth George Peter | Kahama | Zongomera | Zongomera |
| Juma William Mgeja | Kahama | Bokondamoyo | Mhungula |

Kwa mawasiliano zaidi piga simu kwa **Mratibu wa Mahusiano ya Jamii wa Mradi [Cecilia NZEGANIJE - 0699 807 079]**

**MKOA WA TANGA**

| Jina | Wilaya | Kijiji | Kata |
|---|---|---|---|
| Mohamed Ibrahim Mavula | Muheza | Muungano | Mlingano |
| Haruni Levison Nguo | Handeni | Nkale | Kwamatuku |
| Elizabeth George Peter | | | |

Kwa mawasiliano zaidi piga simu kwa **Mratibu wa Mahusiano ya Jamii wa Mradi [Shabani KIMARO, 0623823560, Amanyile MAHALI, 0623823027]**

Waguswa wa Mradi waliotajwa, wanaombwa kuwasiliana na Mradi wa EACOP ili waweze kuonyeshwa stahiki zao, kutia sahihi mkataba wa fidia ili malipo ya fidia yaweze kuendelea kufanyika. Waguswa wanaweza kuwasiliana na Mradi wa EACOP kupitia:

- Kupiga Simu namba ya bure [0800780068]
- Kuandika barua pepe [info.tz@eacop.com]
- Wasiliana na Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa

Waguswa wa Mradi ni lazima wawe na nyaraka muhimu ambazo ni fomu za uthamini walizopewa wakati wa zoezi la uthamini pamoja na vitambulisho. Nyaraka zitakaguliwa na timu ya Mradi kuhakiki usahihi wa utambulisho wao na kuthibitisha kama kweli ni waguswa wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki,
**Waguswa wanaombwa kuwasiliana na Mradi wa EACOP haraka iwezekanavyo.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Madudu katika bima ya afya kamwe yasiachiwe yaendelee

**KATIKA** kuhakikisha Watanzania wengi wanapata huduma za afya bila usumbufu na kwa gharama nafuu, serikali ilianzisha bima ya afya kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na mifuko mingine inayoendeshwa na taasisi binafsi. Lengo la kufanya hivyo ni kuwezesha upatikanaji wa huduma za afya kwa maana ya vipimo na matibabu kuwa rahisi.

Tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000 mfumo huo wa upatikanaji wa huduma za afya umekuwa na unafuu kuliko awali kutokana na ukweli kwamba ni vigumu kwa Watanzania walio wengi kupata matibabu kwa kutumia fedha taslimu. Hiyo inatokana na ukweli kwamba uwezo wa kiuchumi wa wananchi wengi ni mdogo, hivyo ni vigumu kumudu gharama za matibabu ambazo baadhi hugharimu mamilioni ya shilingi.

Licha ya unafuu huo, taasisi zinazotoa huduma za bima ya afya kama vile NHIF, Jubilee na Strategies, zimekuwa pia zikitoa vivutio kupitia vifurushi vyao na watu binafsi, mashirika na taasisi wamekuwa wakichangamkia ili kuhakikisha watu wao wakiwamo wafanyakazi na wategemezi wao wanapata huduma zenye viwango na katika hospitali zenye huduma bora.

Hivi sasa, serikali iko katika mchakato wa bima ya afya kwa wote ambayo mkazo mkubwa ni kuona kila Mtanzania anapata huduma za matibabu katika hospitali za umma na binafsi. Kupitia mpango huo ni imani kwamba wananchi wengi watapata unafuu mkubwa katika huduma za matibabu zikiwamo za vipimo, matibabu na dawa tofauti na sasa ambapo watu wengi wanakosa kutokana na hali zao za kipato kuwa duni.


Pamoja na nia nzuri ya serikali kuwa Watanzania wengi wapate huduma bora, kumekuwa na matumizi mabaya ya kadi za matibabu za NHIF. Wako baadhi ya wanachama wasio waaminifu, wamekuwa wakitoa kadi zao kwa watu wasiostahili na kupata matibabu kinyume cha makusudi halisi ya mfumo huo.

Hiyo ilibainika hivi karibuni baada ya NHIF kufanya uhakiki wa wanachama na utoaji wa huduma za matibabu kwa wanufaika vituoni. Matokeo ya uhakiki huo yamebaini kuwapo madudu mbalimbali yakiwamo wanachama kuazimana kadi ili kupata matibabu. Imebainika kuwa wanachama 1,346 wameazimana kadi ili kupata matibabu na zingine 3,589 zilizokiuka masharti na miongozo zimezuiwa kutumika tena. Kutokana na madudu hayo, NHIF imetangaza kuchukua hatua dhidi ya waliobainika kufanya udanganyifu zikiwamo kusitisha mikataba 48 baina yao na watoa huduma, kuwaripoti watumishi 139 wa sekta ya afya katika mamlaka zao za ajira ikiwamo mabaraza yao ya kitaaluma ili wachukuliwe hatua stahiki. Kadhalika, NHIF imesitisha uanachama kwa waajiri 88 ambao ni watoa huduma binafsi na wafanyakazi wao waliobainika kutumia vibaya kadi za matibabu kwa manufaa binafsi.

Udanganyifu uliofanywa katika matumizi ya kadi za bima ya afya za NHIF ni ukwamishaji wa jitihada njema za serikali katika kuhakikisha Watanzania wanapata huduma za matibabu kupitia mpango wa bima. Kwa maneno mengine, wahusika waliofanya vitendo hivyo ni wahujumu wa mpango wa serikali wa kuleta mapinduzi katika masuala ya afya hususan matibabu kupitia bima ili kutoa unafuu kwa Watanzania.

Kwa uhakiki uliofanyika na kubainika kwa madudu hayo, NHIF inastahili pongezi kwa kuwa imetoa mwanga juu ya nini kinachoendelea katika matumizi ya kadi hizo. Pia hatua zilizochukuliwa ni mwafaka kwa sababu zitasaidia kukomesha tabia za baadhi ya watu wanaokwamisha mpango wa matibabu kwa kutumia bima ya afya. Aidha, hatua zaidi zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya wahusika ikiwamo kufikishwa katika vyombo vya sheria ili kuwa fundisho kwa watu wengine wenye tabia kama hizo. Ni imani kwamba hatua kali zikichukuliwa dhidi ya wanaohujumu jitihada za serikali katika kuboresha huduma za afya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Zingatieni ushauri kitaalamu kulinda figo

**ASILIMIA** saba ya Watanzania wanaishi na ugonjwa wa figo, ambao unaelezwa kuwa ni miongoni mwa magonjwa sugu yasiyoambukiza ambayo chanzo chake kinahusiana na ulaji usiofaa na mitindo ya maisha.

Ugonjwa wa figo pia unatajwa kuwa huingia katika mwili wa binadamu kimya kimya bila ya kuonyesha dalili za awali na kwamba dalili hujitokeza wakati ugonjwa ukishakomaa.

Kutokana na hali hiyo, jamii inashauriwa kujenga tabia ya kufanya uchunguzi wa figo mara kwa mara na kufuata ushauri wa wataalamu wa afya ili kuwa salama zaidi dhidi ya ugonjwa huo.

Kwa kuwa inaelezwa kwamba chanzo chake ni mtindo wa maisha unaohusisha ulaji na unywaji, ninadhani ni vyema kila mmoja wetu kuwa makini ili kuepuka ugonjwa huo.

Hivi karibuni, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Profesa Mohamed Janabi, alisema takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 90 ya wagonjwa wanaopata matibabu ya figo MNH-Upanga na Mloganzila wamepata changamoto ya figo kutokana na shinikizo la juu la damu.

Na kwa hali hiyo, wito wake kwa jamii ijikite katika kujikinga na maradhi yasiyoambukiza, kwa kuwa gharama za kutibu ni ghali, akitolea mfano kuwa mgonjwa mmoja wa figo anayefanyiwa huduma ya kuchuja damu, gharama yake ni Sh. 180,000 kwa awamu moja.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, mgonjwa anahitaji kufanyiwa huduma ya kuchuja damu kwa awamu tatu kila wiki, hali ambayo inaonyesha kuwa gharama ni kubwa hasa kwa watu wa kawaida.

Ninadhani maelezo hayo ya wataalamu wa afya yangetosha kutufanya kuwa makini kulinda afya zetu kutokuwa na uzito uliopitiliza, matumizi holela ya dawa, tabia ulaji usiozingatia ushauri wa wataalamu hao.

Kwa baadhi ya watu, ninaamini kwao ni jambo la kawaida kwao kutozingatia ushauri wa wataalamu wa afya, wanaweza kujisikia kuumwa na kwenda katika maduka ya kununua dawa na kuanza kutumia.

Mtindo huo unapingana na maelekezo ya wataalamu wa afya ambao wanashauri kutotumia dawa holela, hivyo ingefaa kufuata ushauri huo ili kuepuka magonjwa ukiwamo huo wa figo.

Lakini unywaji, uvutaji, ulaji usiozingatia ushauri wa wataalamu wa afya na kubweteka bila kufanya mazoezi, navyo ni tatizo, ingefaa kuchukua hatua mapema ili kuepuka gharama za kuchuja damu.

Hayo ndio wataalamu wa afya wanashauri kuyazingatia, ikiwamo kula vyakula mchanganyiko kwa kiasi kulingana na mahitaji ya mwili yanayotokana na kazi ambazo mtu anafanya.

Kudhibiti uzito wa mwili kwa kufanya mazoezi na kuepuka vyakula vilivyopikwa kwenye mafuta mengi na vinywaji vilivyoongezwa sukari kama soda aina zote, juisi za makopo.

Lakini wanaelekeza kuepuka uvutaji wa sigara na mazao yote ya tumbaku, kwa kuwa husababisha mishipa kusinyaa, kuepuka dawa za maumivu kama hakuna ushauri wa madaktari.

Aidha, unywaji wa maji mengi angalau lita moja na nusu kwa siku ndio unaoshauriwa na kufanya uchunguzi wa figo angalau mara moja kwa mwaka, ili kujua maendeleo ya afya.

Aidha kwa watu ambao tayari wana ugonjwa huo, wanashauriwa kudhibiti magojnjwa ya kisukari kwa kufuata ushauri na matumizi ya dawa kama alivyokuelekezwa mtaalamu wa afya.

Jambo la muhimu hapa ni kuzingatia ulaji unaofaa, na kuepuka kukaa na njaa, lakini pia wanatakiwa kudhibiti shinikizo la damu kwa kufuata ushauri na dawa kama alivyoelekeza daktari.

Vilevile wanatakiwa kupata matibabu sahihi ya ugonjwa wa mawe kwenye figo na tezi dume, kudhibiti kiwango cha maji na vimiminika vingine kama ilivyoshauriwa na daktari na kuepuka matumizi ya chumvi.

HABARI KITAIFA

# Viongozi wa dini kupambanana wanaoleta chokochoko

**Na Beatrice Shayo**

JUMUIYA ya Maridhiano Tanzania (JMAT), imesema viongozi wa dini hawatakubali kuona mtu yeyote anaichezea amani ya Tanzania kwa kuanzisha chokochoko zisizokuwa na msingi.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Shekhe Alhad Mussa Salum, alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Maonyesho ya 47 ya Biashara Kimataifa (Sabasaba) yanayoendelea katika viwanja vya Mwalimu Nyerere.

"Hatutakubali mtu yeyote kuichezea amani ya nchi yetu kwa kuleta chokochoko yoyote ile...sisi kama viongozi wa dini hatutakubali tupo pamoja kuisaidia serikali katika yale ambayo ni mema wanayowafanyia Watanzania," alisema Shekhe Salum.

Alisema kikubwa wanachokifanya ni kuiombea nchi iendelee kuwa na amani zaidi pamoja na viongozi na serikali kwa ujumla.

Aidha, alisema biashara yao kubwa waliyoileta katika maonesho hayo ya Sabasaba ni kuuza amani ya nchi kwa Watanzania.

"Wakati tunajiandaa katika banda letu kuna majirani wetu hawa Wachina na wengine wageni walikuwa wanatushangaa kuona banda letu limejaa biblia na misahafu, wanatuuliza sisi tunapata faida gani? Sisi tumeleta biashara humu nyie mnakaa mnafanya biashara gani," alisema.

"Tuliwajibu na kuwaambia sisi biashara yetu ni amani na utulivu ndicho ambacho tunauza humu Sabasaba. Amani na utulivu umewafanya wao kufanya biashara sisi biashara yetu haina faida. Faida yetu ni kuona Tanzania inabaki kuwa salama na kuwa na mahusiano mazuri kati ya wana dini hii ndiyo biashara ambayo tunaifanya hapa."

Alisema biashara ya kuwauzia Watanzania amani waone thamani yake imewafanya waonekane wapo tofauti na mabanda mengine.

"Mabanda yote yapo kibiashara zaidi, lakini sisi tumejikita kuuza amani na utulivu. Tunawauzia Watanzania tunawaambia wanunue hii amani wachague amani na utulivu katika nchi yetu ndiyo maana tupo hapa watu wa madhehebu mbalimbali tunapigania mahusiano haya," alisema Shekhe Salum.

Aidha, alisema anaipongeza Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) kwa namna walivyojipanga katika maonesho ya mwaka huu kuwa ni mazuri na viongozi wengi wametembelea mabanda kujionea bidhaa mbalimbali.

Alisema alivyotembelea baadhi ya mabanda ameona namna Watanzania walivyojipanga na kujisimamia wao wenyewe na kutoa huduma zenye ubora.

"Watanzania tupo vizuri tunaweza kusimamia mambo yetu wenyewe hili ni jambo jema tumejifunza mambo mengi katika mabanda tuliyotembelea," alisema.

Alimpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapo na mazingira mazuri na serikali yake katika suala zima la amani kwa kuwa kama isingekuwapo maonesho hayo yasingefanyika.

# Ujenzi Bwawa la Nyerere wafikia asilimia 90

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba ameongoza viongozi wa Baraza la Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Baraza la Maaskofu la Kanisa Katoliki (TEC), kutembelea bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (JNHPP).

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Waziri Makamba alisema ujenzi umefikia asimilia 90 huku akibainisha kuwa kumekuwa na mwenendo mzuri wa mtiririko wa maji yanayoingia katika bwawa hilo.

Alisema hadi sasa mita za ujazo katika bwawa hilo zimefikia 163.7 za usawa bahari kutoka mita 163.61 alizozitangaza wiki iliyopita jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya mradi huo.

"Maana yake leo tungekuwa tumefunga mitambo ya kuzalisha umeme tungeanza shughuli hii. Lakini mmeona kazi ya kufunga mitambo ya kufua umeme inaendelea pamoja na nyumba ya mitambo hii shughuli yake imefikia asilimia 70," alisema.

Alisema matarajio yao kuona Februari mwakani wakianza majaribio ya kuzungusha mitambo hiyo, kabla ya Juni mwaka 2024 kuanza rasmi shughuli za kuzalisha umeme wa megawati 2,115 utakaoingizwa katika gridi ya Taifa. Katika hatua nyingine, Waziri Makamba aliwashukuru viongozi hao wa dini wakiongozwa na Askofu Lazarus Msimbe anayewakilisha TEC na Askofu Mndolwa wa CCT ambaye ni Askofu wa Anglikana Dayosisi ya Tanga.

Waziri Makamba alisema: "Tunashukuru Mungu ujio wa viongozi hawa wa dini waliouombea mradi na mheshimiwa Rais wetu (Samia Suluhu Hassan). Mradi huu ukikamilika utakuwa na manufaa makubwa kwa Watanzania.

"Mradi wa JNHPP ukikamilika Watanzania hawatasikia kelele za mradi wa Kinyerezi umesimama kwa hiyo hatutokuwa na mgao, haitakuwa hivyo kwa sababu tutakuwa na umeme wa kutosha, labda kutokee changamoto zingine za miundombinu," alisema.

Askofu Dk. Maimbo Mndolwa alisema baada ya kutembea maeneo mbalimbali ya mradi huo ujumbe walioubeba ni kuwahamasisha wauminі kuhifadhi na mazingira, ili kuwezesha maji yanayotoka katika vyanzo mbalimbali kwenda Mto Rufiji.

Alisema baada ya kutembelea wanarudi kutoka kwenye mradi huo wakiwa na moyo na ari mpya ya kuhamasisha wananchi wananchi kutunza na kuyahifadhi mazingira.

Mwakilishi wa TEC, Askofu Msimbe aliishukuru serikali kutoa wazo la viongozi wa dini kutembelea mradi huo mkubwa wa kitaifa, akisema wametambua thamani ya viongozi katika shughuli za maendeleo ya nchi.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.
(Together we can build a better life)

PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

PURSUANT TO REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014 AND REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER PROTECTION 2019.

| | TZS | | | USD | |
|---|---|---|---|---|---|
| **A. SAVINGS BANK** | | | | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | | | FREE | | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | | | FREE | | FREE |
| 3. A/C Statement Charges | | | | | |
| a) Monthly | | | FREE | | FREE |
| b) Interm | | TZS | 4,300.00 | $ | 5.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | | | FREE | Up to 5000 | FREE |
| | | | | Above 5000 | 0.26% |
| 5. Cash Deposit Charges | | | FREE | | FREE |
| 6. Balance Confirmation certificate | | TZS | 12,800.00 | $ | 6.00 |
| 7. A/c Closure charges | | TZS | 12,800.00 | $ | 13.00 |
| 8. Activation of Dormat A/c | | TZS | 5,100.00 | $ | 6.00 |
| **B. CURRENT ACCOUNT** | | | | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | | | FREE | | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | | | FREE | | FREE |
| 3. A/C Statement Charges a) Monthly | | TZS | 4,300.00 | $ | 5.00 |
| b) Interm | Fixed | TZS | 4,300.00 | Fixed | $5.00 |
| | plus For each page | TZS | 500.00 | For each page | $1.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MILLION | | FREE | Upto 5000 | FREE |
| | ABOVE 25 MILLION | | 0.11% | 5000 to 10,000 - | 0.26% |
| | | | | Above 10,000 | 0.43% |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO | | FREE | Upto 10,000 | FREE |
| | ABOVE 50 Million | | 0.11% | > 10,000- | 0.26% |
| 5. Balance Confirmation certificate | | TZS | 21,200.00 | | $13.00 |
| 6. Stop Payment Charges | | TZS | 25,500.00 | | $13.00 |
| 7. Cheque Clearing Charges | | | | | |
| a) Inward | | TZS | 1,300.00 | | $1.00 |
| b) Outward | | | FREE | | FREE |
| 8. Cheque Return Charges | | | | | |
| a) Inward | | TZS | 25,500.00 | | $13.00 |
| b) Outward | | TZS | 25,500.00 | | $13.00 |
| 9. A/c closure charges | | TZS | 21,200.00 | | $17.00 |
| **C. MOBILE BANKING CHARGES** | | | | | |
| **1. Cash Withdrawal** | | | | | |
| Upto 100,000 | | TZS | 1,700.00 | | NA |
| 101,000 to 200,000 | | TZS | 2,600.00 | | NA |
| 201,000 to 400,000 | | TZS | 4,300.00 | | NA |
| 401,000 to 600,000 | | TZS | 5,100.00 | | NA |
| 601,000 to 999,000 | | TZS | 6,800.00 | | NA |
| **2. Funds Transfer/Mobile Wallet** | | | | | |
| Upto 100,000 | | TZS | 500.00 | | NA |
| 101,000 to 250,000 | | TZS | 900.00 | | NA |
| 251,000 to 500,000 | | TZS | 1,700.00 | | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | | TZS | 4,300.00 | | NA |
| 1,001,000 TO 10 Mn | | TZS | 8,500.00 | | NA |
| **Mobile Banking Services** | | | | | |
| A) Monthly Subscription Charges | | TZS | 500.00 | | NA |
| B) PIN Request | | TZS | 2,200.00 | | NA |
| **D. LOCKERS RENT YEARLY** | | | | | |
| 1.SMALL | | TZS | 296,700.00 | | NA |
| 2. MEDIUM | | TZS | 508,500.00 | | NA |
| 3. BIG | | TZS | 635,600.00 | | NA |

| E. REMITTANCES | TZS | | USD | |
|---|---|---|---|---|
| 1. TISS | TZS | 8,450.00 | EQUIVALLENT TO TZS 8450 | |
| **2. E Remittances** | | | | |
| Upto USD 1000 or Eq. TZS | TZS | 17,000.00 | $ | 9.00 |
| 1001 to 5000 | TZS | 20,400.00 | $ | 11.00 |
| 5001 to 10000 | TZS | 40,700.00 | $ | 22.00 |
| 10,001 and above | TZS | 84,800.00 | $ | 43.00 |
| **3. SWIFT** | | | | |
| **a) Swift Outward** | | | | |
| Upto 5,000 | | NA | $ | 39.00 |
| 5,001 to 10,000 | | NA | $ | 51.00 |
| above 10,000 | | NA | $ | 77.00 |
| **b) Swift Inward** | | | | |
| Upto 5,000 | | NA | $ | 11.00 |
| 5,001 to 10,000 | | NA | $ | 16.00 |
| above 10,000 | | NA | $ | 26.00 |

| F. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES | TZS | | USD | |
|---|---|---|---|---|
| 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - TZS | 21,200.00 | Upto 5,000 - | $85.00 |
| | 5Mio to 10 Mio - TZS | 169,500.00 | 5000 to 10,000 - | $170.00 |
| | 10 Mio to 25mio - TZS | 339,000.00 | Upto 20,000 - | $255.00 |
| | 25 mn to 500 mio - | 1.28% | 20,000 to 500,000 - | 1.28% |
| | >500mio--* (*minimum 7.5mio) | 1.06% | >500,000--* (*minimum 7,500) | 1.06% |
| 2. Documentation Charges | Upto 100 MILLION | FREE | Upto 50,000 FREE | |
| | >100 Mio (-Min 300,000) | 0.26% | >50,000 - (Min 150) | 0.26% |
| 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - TZS | 21,200.00 | Upto 20,000 - | $255.00 |
| | 5 Mio to 10 Mio - TZS | 169,500.00 | 20,000 to 500,000 - | 1.53% |
| | 10Mio 25mio - TZS | 381,400.00 | >500,000--* (*minimum 9000) | 1.28% |
| | 25 mn to 500 mio - | 1.53% | | |
| | >500mio--* (*minimum 9mio) | 1.28% | | |
| 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio - TZS | 21,200.00 | Upto 50,000 | $22.00 |
| | >100 mio - TZS | 42,400.00 | >50,000 | $43.00 |
| 5.Credit Reference Report Charges from D&B Tanzania | TZS TZS | 101,700.00 | | $43.00 |
| 6.Pre-payment penalty | Calculated as %ge pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders | 1.70% | of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders | 1.70% |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | | | |
| Bonds & Guarantees | ( Min TZS 75,000) | 1.02% | | 1.02% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | per quarter (Min TZS 75,000) | 0.43% | | 0.43% |
| **H. LETTER OF CREDIT** | | | | |
| **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | | | |
| Opening commission | NA | | ( Min $ 200) | |
| LC amendment Commission | NA | | ( Min $50 max 350) | 1.02% |
| Swift charge for LC opening | NA | | | 0.34% |
| Swift charge for other message/amendments | NA | | | $34.00 |
| Extensions - Commissions | NA | | ( Min $200) | $34.00 |
| LC cancellation charges | NA | | ( Min $200) | 1.02% |
| Non payment of Bills on due date | NA | | Till Payment | 1.02% |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | | | |
| Advising commission | NA | | | $119.00 |
| Confirmation Commission | NA | | ( Min $150) | 0.43% |
| Negotiating bills under LC | NA | | (Min $75+cuourier+int) | 0.43% |
| Reimbursement claim paid | NA | | ( Min$75) | 0.43% |
| Extensions - Commissions | NA | | ( Min $200) | 1.02% |
| Collection of Export LC | NA | | (Min $75+cuourier+int) | 0.43% |
| Amendments | NA | | | $64.00 |

OTHER DISCLOSURES(VIAMBATANISHI)

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 5 | 5 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 3.00% | 1.00% |

**i. Fixed Deposits of TZS**

| Amount in TZS | up to TZS 50 M | TZS 50 M-100M | Above 100 M |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 3.50% | 4.50% | 5.50% |
| 91-180days | 4.50% | 5.50% | 6.50% |
| 181-364 days | 5.50% | 7.00% | 7.50% |
| 1 year and above | 8.00% | 8.25% | 8.50% |
| 2 Years and Above | 8.00% | 9.00% | 9.50% |

**ii. Fixed Deposits of USD**

| Amount in USD | up to USD 50,000 | USD 50,000 -USD 100,000 | Over USD 100,000 |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 1.50% | 2.25% | 2.50% |
| 91-180days | 2.25% | 2.50% | 3.25% |
| 181-364 days | 3.00% | 3.50% | 4.00% |
| 1 year and above | 3.75% | 4.25% | 4.75% |
| 2 Years and Above | 4.00% | 4.75% | 5.00% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| SALMA MRISHO | HEAD TREASURY AND TRADE FINANCE | SIGNED | 11-July-23 |
| KAUSHENDRA TIWARI | GM-CREDIT | SIGNED | 11-July-23 |
| VIBHUTI CHOUDHARY | DEPUTY CEO | SIGNED | 11-July-23 |

217495202

# NSSF yajigamba kulipa mafao mpaka miaka 40 ijayo

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Balozi mstaafu Ali Iddi Siwa, amesema mfuko ni endelevu na uhai wake ni kwa miaka 40 ijayo.

Alisema hayo juzi wakati alipotembelea banda namba 13 la ushirikiano baina ya NSSF na PSSSF katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara 'Sabasaba' yanayoendelea katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.

"Napenda kuwahakikishia wanachama kuwa mfuko umefikia thamani ya shilingi trilioni 7.1 kiwango ambacho ni kikubwa, hivyo nawatoa wasiwasi wanachama kuwa NSSF ina uwezo wa kulipa mafao mbalimbali kwa kipindi cha miaka 40 inayokuja mbele," alisema Balozi Siwa.

Pia, alisema mfuko unatekeleza majukumu makuu manne ambayo ni kuandikisha wanachama kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, kukusanya michango, kuwekeza na kulipa mafao. Mfuko unaendelea kuboresha mifumo mbalimbali ikiwamo ya TEHAMA, utendaji na kuwekeza ili kuhakikisha miaka 40 inapita.

Kadhalika, wanachama waliopo katika mfuko hivi sasa ni zaidi ya milioni mmoja na wanatarajia kufikisha wanachama hai zaidi ya milioni mbili kutokana na kasi ya ukuaji wa sekta binafsi ambao mfuko unapata wanachama wengi.

"Napenda kuipongeza serikali kwa kufungua nchi na kutengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji, kwa upande wetu NSSF tunapata wanachama wengi kupitia uwekezaji unaofanywa kwenye maeneo mbalimbali," alisisitiza.

Kuhusu uwekezaji wa mfuko, alisema kazi inayofanywa na mfuko inaendelea kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa na kwa sasa wamedhamiria kuwekeza jijini Dodoma.

Pia, Mfuko unawekeza katika miundombinu ikiwamo Daraja la Nyerere, Kigamboni ambalo limekuwa msaada mkubwa kwa wananchi ambao hivi sasa wanavuka kwa kutumia bando la siku, wiki au mwezi kwa gharama nafuu.

Alisema katika Jiji la Mwanza, Mfuko umefanya uwekezaji mkubwa wa hoteli ya kitalii yenye hadhi ya nyota tano ambayo inaenda kufungua fursa mbalimbali katika mkoa huo ikiwamo shughuli za utalii.

Mfuko unatoa huduma zake zote katika maonesho hayo ikiwamo uandikishaji wanachama kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, elimu kuhusu mafao, uwekezaji pamoja na fursa za nyumba na viwanja ambavyo vinauzwa katika maeneo mbalimbali.

Aliwaalika wanachama na wananchi wote kutembelea bando la NSSF ili waweze kunufaika na fursa mbalimbali ikiwamo kujiunga na kuchangia katika Mfuko.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Balozi mstaafu Ali Idi Siwa, akimkabidhi Joyce Sungura, kadi ya uanachama wa NSSF baada ya kujiunga wakati alipotembelea banda lao katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara 'Sabasaba'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TBA kushirikiana na sekta binafsi kufanyakazi

**Na Beatrice Shayo**

WAKALA wa Majengo Tanzania (TBA) upo katika hatua za mwisho kuanza kufanya kazi kwa kushirikiana na sekta binafsi kama alivyoagiza Rais Samia Suluhu Hassan.

Hayo yalisemwa juzi jijini Dar es Salaam na Mtendaji Mkuu wa TBA, Daudi Kondoro, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea banda lao lililopo katika Maonyesho ya 47 ya Biashara Kimataifa (Sabasaba).

Alisema wakati wa uzinduzi wa nyumba 644 za Magomeni, jijini Dar es Salaam kulikuwa na maelekezo yaliyotolewa na Rais Samia kwa TBA kuwa imefike wakati wanatakiwa kufanya kazi na sekta binafsi.

Kondoro alisema jambo hilo walilichukua na walilifanyia kazi ambalo ni kuhakikisha wanauhisha tamko la uanzishwaji wa Wakala wa Majengo Tanzania. "Kuuhisha maana yake ifike wakati tuanze kufanyakazi na sekta binafsi tayari tumeanza kulifanyia kazi tumeishirikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora," alisema.

Kwa sasa alisema wapo katika hatua za mwisho za kukamilisha makubaliano hayo waanze kushirikiana na sekta binafsi.

"Tupo kwenye hatua za mwisho kukamilisha jambo hilo matarajio yetu kasi itakuwa kubwa kwa sababu tunaishirikisha sekta binafsi," alisema Kondoro.

Aidha, hakuna mradi ambao umekwama na TBA ilianzishwa kwa ajili ya kuhakikisha wanajenga nyumba kwa ajili ya viongozi na watumishi wa umma.

Alisema miradi mingi ipo kwenye hatua za mwisho za utekelezaji na bajeti ya mwaka huu iliyopitishwa wataanza ujenzi katika mikoa ya Mwanza, Arusha na Dar es Salaam.

"Matarajio yetu tutakuwa na mambo makubwa kuna ujenzi mkubwa utajengwa Arusha na upo mradi mwingine Temeke kota tutajenga block saba na kila block itakuwa na familia 144 tumeshaanza na block moja," alisema.

# Posta yaja na duka mtandaoni

**Na Restuta James**

SHIRIKA la Posta Tanzania limeboresha huduma zake nne ikiwamo ya duka mtandao (e-shop), inayowawezesha wajasiriamali kuuza bidhaa zao katika nchi 192 duniani.

Aidha, limeanzisha huduma ya posta kiganjani ambayo namba ya simu inatumika kama sanduku la barua.

Akizungumza na Nipashe katika maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa yanayoendelea katika viwanja vya Sabasaba, Mratibu wa shughuli za mikoa, Khamis Swedi, alisema mjasiriamali anayeweka bidhaa kwenye duka hilo, anaweza kumuuzia mteja kwa fedha ya nchi husika na kwa lugha yake.

Alisema duka mtandao linatafsiri ya zaidi ya lugha 10 ikiwamo Kichina, Kiarabu, Kiswahili, Kiingereza, Kireno, Kirumi, Kispaniola, Kihausa, Kitaliano na Kifaransa.

Alisema kwa sasa linawasajili wajasiriamali bila malipo na kwamba shirika hilo linapata asilimia mbili ya mauzo ya bidhaa.

Swedi alisema ili mjasiriamali aweze kuingia katika soko la kimataifa ni lazima bidhaa zake ziwe zimethibitishwa ubora na mamlaka husika kama sheria zinavyotaka.

Alifafanua kuwa katika kipindi cha Sabasaba, wamefanikiwa kusajili wajasiriamali 32.

"Kikubwa ni kwamba mjasiriamali akijisajili kwetu anauza kwenye soko kubwa yaani hizo nchi 192, lakini mteja hapati usumbufu wa kuijua bidhaa kwa sababu anaipata kwa bei ya nchi yake na kwa lugha yake. Yaani mjasiriamali akiweka bei ya Shilingi, mtu aliyepo China ataipata kwa fedha ya China kwa thamani ya bei iliyopo dukani," alisema.

Kuhusu posta kiganjani, Swedi alisema shirika hilo limeanzisha 'aplikesheni' ya posta kiganjani ambayo inahuduma zote za posta.

"Hivi sasa mtu anaweza kupata sanduku la barua kwa namba yake ya mkononi. Maboresho yanayoendelea yatamfanya mteja mwenye sanduku hili kupata taarifa ya barua yake inapotoka hadi inamfikia, lakini pia mteja ataweza kufuatilia (track), mzigo wake," alisema.

Alisema posta inasafirisha pia mizigo mikubwa na vifurushi ndani na nje ya nchi, zikiwamo sampuli za maabara kutoka sehemu mbalimbali hadi maabara kuu ya Taifa.





## Madini yakusanya bil. 2.6/- 2022/23

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

OFISA Madini Mkazi (RMO) wa Mkoa wa Kimadini wa Mirerani, Menard Msengi, amesema ofisi hiyo imefanikiwa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 2.611 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Taarifa ya makusanyo hayo ilitolewa jana na Msengi, wakati akiwasilisha taarifa hiyo kwa Waziri wa Madini, Dotto Biteko.

Alisema makusanyo ya fedha hizo kwa mwaka huo wa fedha ni sawa na asilimia 52.23 ya malengo waliyowekewa.

Alitaja baadhi ya sababu zilizochangia wasifikie malengo ni shughuli za kijiolojia mashapo, kuwa katika kina kirefu hivyo migodi mingi kutumia muda mrefu kufanya utanuzi na uwekezaji mdogo.

"Pia, ukosefu wa teknolojia za kisasa kwa wachimbaji wadogo, mvua ziliathiri miundombinu ya uchimbaji na usafirishaji madini ujenzi, ukosefu wa miundombinu ya umeme kwenye baadhi ya machimbo ya vito," alisema Mhandisi Msengi.

Pia alitaja mikakati waliyonayo ni kuongeza vituo vya madini ujenzi, kulingana na jiografia ya Wilaya ya Simanjiro, utoaji wa elimu kwa wafanyabiashara wa madini wasio rasmi ili waweze kukata leseni, kufuatilia na kusimamia kwa kina miradi ya ujenzi wa viwanda vya madini.

Alisema soko la madini linaendelea vizuri, hadi sasa lina wafanyabiashara wakubwa 27 na ujenzi wa soko litakalotumika kuwahudumia wafanyabiashara wa madini ya tanzanite, unaendelea chini ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Alisema eneo la kitalu C, kampuni ya Franone Mining and Gems LTD, imefanya uzalishaji wa kilo 146 za madini ya tanzanite.

Vilevile, alisema kiasi hicho cha madini ya tanzanite kilogramu 146 kilichozalishwa na Kampuni ya Franone Mining Ltd kina thamani ya zaidi ya Sh. milioni 709, kitaiwezesha serikali kupata zaidi ya Sh. milioni 49.

# WVT yasaidia gharama chakula cha shule

**Na Daniel Sabuni,** LONGIDO

SHIRIKA la World Vision Tanzania (WVT), limewatua mzigo wa kuchangia gharama za chakula shuleni wazazi na kupunguza tatizo la utoro, baada ya kuzipatia shule za msingi 30 za Wilaya ya Longido mkoani Arusha, tani 85 za chakula aina ya mahindi na maharage.

Aidha, limetoa na kukabidhi lita 5,480 za mafuta ya kupikia kwa shule hizo, ambayo yana thamani ya Sh. milioni 175.

Akizungumza jana, wakati wa kukabidhi misaada hiyo kwa walimu na wanafunzi wa Shule za Msingi Engushei na Ketumbeine, Mratibu wa Mradi wa Ketumbeine AP, Peruth Daudi, alisema fedha za kugharamia misaada hiyo zimefadhiliwa na Shirika la World Vision nchini Marekani.

Peruth, alisema jumla ya shule 24 zimefikiwa kupata msaada huo katika Tarafa ya Ketumbeine, ambako kuna shule nne za awali na mbili za msingi.

Alizitaja shule za Tarafa ya Ketumbeine zilizofaidika, kuwa ni Ketumbeine Shule ya Msingi, Olopolosek, Mangula, Magadini, Gilai Bomba, Lumbwa, Esokonoi na shule za Msingi Longido. Wakati Tarafa ya Longido ni Shule ya Msingi Kimokoa.

"Chakula kilichotolewa ni tani 57, sawa na magunia 1,140 ya mahindi, tani 28 za maharage, ambazo ni sawa na magunia 281, lakini yamo mafuta ya chakula ndoo 274 (zote zikiwa na ujazo wa lita 20 kila moja).

Mratibu huyo, alisema World Vision imefikia uamuzi huo kutokana na kuguswa na tatizo la ukosefu wa chakula kwenye shule hizo. Tatizo hilo lilisababishwa na ukame uliotokea wa mwaka jana, na wazazi kushindwa kumudu kuchangia chakula na kuathiri mahudhurio.

"Chakula hiki kitafaidisha watoto 11,726 katika shule hizo, tunategemea ndani ya miezi minne ya chakula kilichotolewa, mahudhurio yatapanda kutoka asilimia 58 ya sasa mpaka tisa," alisema.

Mwaka jana, Shirika hilo kupitia programu ya kusaidia vyakula shuleni, liligawa chakula kwa watoto 10,272 kwenye shule zote za Tarafa ya Ketumbeine, ambacho kilikuwa na thamani ya Sh. milioni 227.

Alisema chakula hicho katika muda usiozidi miezi sita, kilisaidia kuongeza mahudhurio kutoka asilimia 56 na kufikia 99 mpaka 112.

Akizungumza baada ya kugawiwa chakula kwa niaba ya wanafunzi wenzake, mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Msingi Longido (mwenye ulemavu wa kutoona), Minyali Ngeli, alishukuru kupata chakula hicho ambacho kitawasaidia kupata nguvu ya kusoma vyema wakati wa mchana.

"Tunapokosa mlo wa mchana, wengi wanasinzia wakati Mwalimu akifudisha au wakati wa kujisomea wengi tunasinzia, tunawashukuru Worldvision kwa msaada huu," alisema Ngeli.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marco Ng'umbi, akizungumza baada ya makabidhiano hayo, alilishukuru shirika hilo kwa msaada huo, huku akiwaahidi atasimamia matumizi sahihi ya chakula hicho ili kisaidie kwa muda uliopangwa na kuleta tija kwenye elimu.

"Shirika hili ni mkono wa pili wa serikali katika kuwahudumia wananchi. Nasikia mnamaliza muda wenu mwezi Septemba mwaka huu hapa Longido, nawaomba na nitaandika barua rasmi kwa uongozi wa shirika muendelee kuleta miradi mingine hapa," alisisitiza.



Kamishna wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji Hasina Omari (wa pili kulia), akitoa maelekezo ya uchaguzi kwa wasimamizi na maofisa uchaguzi wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga juzi, baada ya kufunga mafunzo ya wasimamizi wakuu, wasaidizi na makalani watakaosimamia uchaguzi mdogo wa udiwani Kata ya Potwe wilayani humo leo. Wengine ni ofisa uchaguzi wa wilaya hiyo, Zainabu Saidi (kushoto), Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo ambaye ndio msimamizi mkuu wa uchaguzi, Dk. Jumaa Mhina (wa pili kushoto) na Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Mpigakura, Monica Mnanka. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kasi ya teknolojia kubadili ufundishaji shuleni

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Tekinolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema kutokana na kasi ya ukuaji wa teknolojia duniani, inakoelekea hakutakuwa na mwalimu atakayeingia darasani na kuandika kwenye ubao, badala yake kutatumika teknolojia kuwafundisha na kuwafikirisha wanafunzi wajifunze mpaka waelewe wenyewe.

Prof. Mkenda, alikuwa akizungumza jana na menejimenti ya Kituo cha Sayansi cha STEM Park kilichoko jijini Tanga, alipokwenda kukagua maendeleo yake.

"Nimetembelea kituo hiki cha Sayansi ili kuona maendeleo ya elimu ya Sayansi na Teknolojia. Hapa nimeona vitu vizuri vyofundisha kupitia teknolojia; tunakoelekea hakutakuwa na mwalimu atangia darasani na kuandika kwenye ubao, bali watakuwa wakitumia teknolojia.

"Hii STEM Park ni kitu kimoja cha umuhimu sana, ambacho kitakwenda kuchochea utundu na uelewa wa vijana. Hapa nitoe pongezi kwa Halmashauri ya Jiji la Tanga, kwa kutoa eneo hili ambalo wenzetu wamejenga Park hii na kuwawezesha vijana wetu."

Baada ya ukaguzi huo, Waziri Mkenda, alisema wizara yake ina mpango wa kujenga vyuo vingi nchini ili watoto wengi wapate kujifunza na kwa kuanzia kutajengwa kituo kikubwa jijini Dodoma, ambacho kitakuwa cha mfano, kabla ya kujengwa kila mkoa.


Awali, Mkurugenzi wa Kituo cha Sayansi cha STEM Park, kilichoko chini ya Project Inspire, Dk. Lwidiko Mhamilawa, alisema wanafundisha wanafunzi kutokana na udadisi wao wa kiakili ya sayansi na kuwawezesha mpaka kufikia kuwa wana sayansi halisi.

"Hii ni kufundisha kupitia mbinu mbalimbali ikiwamo miradi, lakini kuandaa mazingira mazuri ya kujifunzia kama vile kujenga STEM Parks, ambazo kwa sasa zipo hapa Tanga na Dar es Salaam. Sasa pamoja na kuwapatia fursa na kuwashikilia tangu wakiwa wadogo, tunahakikisha wanajifunza na kupata hamasa ya kuipenda sayansi.

"Kwa nchi zilizoendelea takribani asilimia 60 mpaka 70 ya mapato yao yanatokana na teknolojia, sayansi, uhandisi na mahesabu. Na ili Tanzania tuweze kufika huko, tunahitaji wanataaluma wengi. Kwa hiyo, ndiyo maana tunafanya hivi kwa miaka minane sasa."

Kwa mujibu wa Dk. Mhamilawa, tangu kuanzishwa kwa kituo hicho mwaka 2021, wamekuwa wakipata wanafunzi tofauti kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji la Tanga, na hadi sasa, tayari wameshatoa mafunzo kwa watu 30,000.

Naye Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Amos Nungu, alisema kama ilivyokuwa kwa COSTECH, STEM pia inasaidia kuhamasisha na kujifunza masuala ya sayansi, teknolojia na hesabu kwa ufanisi zaidi na kujenga uelewa kwa wanafunzi.





# Waomba jokofu kuhifadhi miili

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

BAADHI ya wananchi kutoka Kata ya Isaka, Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama mkoani Shinyanga wameiomba serikali pamoja na wadau mbalimbali wa afya kusaidia upatikanaji wa jokofu kwa ajili ya kuhifadhia miili ya wapendwa wao katika Kituo cha Afya Isaka.

Walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na Nipashe na kueleza kuwa licha ya serikali kutatua kero ya huduma za afya bado wanakabiliwa na ukosefu jokofu na kuwalazimu kufuata huduma hiyo katika hospitali ya wilaya.

Joackim Manyande, mkazi wa kata hiyo alisema inawalazimu kusafiri umbali mrefu kuelekea katika hospitali ya wilaya ili kupata huduma na hutumia gharama kubwa.

"Tunashukuru kwa kupata kituo cha afya karibu, lakini kwa sasa ikihitajika huduma ya kuhifadhi maiti tunalazimika tena kulipia usafiri kuelekea katika hospitali ya wilaya na kuingia gharama nyingine tofauti, tunaomba serikali na wadau watusaidie kupata huduma hii karibu," alisema Mariamu Shija mkazi wa kata hiyo.

Akizungumza wakati wa kupokea vitanda na magodoro 50 pamoja na shuka 200 vyenye thamani ya Sh. milioni 68.9 kutoka katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Mganga Mfawidhi wa kituo hicho Dk. Immaculata Matete, alithibitisha kuwapo kwa kero hiyo na kueleza kuwa hupewa rufani kupeleka wapendwa wao katika hospitali ya wilaya kwa ajili ya kuhifadhiwa.

Alisema kuwa kituo hicho kinahudumia watu 32,000 kutoka katika kata za Isaka, Jana, Igusule, Mwakata, Nyashimbisigiri na kuongeza kuwa kwa siku wanahudumia zaidi ya wagonjwa 50 na uhitaji wa jokofu ni muhimu zaidi kupunguza gharama zisizo za lazima.

Meneja Uhusiano na Mawasiliano kutoka TPA Makao Makuu, Nicodemus Mushi, alisema hutoa faida ya fedha wanazozipata kupitia bandari ya nchi kavu ya Isaka ambako kwa mwaka jana waliotoa mabati 315 kwenye jengo la wodi ya mama na mtoto, wametoa shuka, godoro na vitanda vyote vikiwa na thamani Sh. milioni 68.9.

# Wananchi wajenga kituo cha polisi kukabili uhalifu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKAZI wa Kata ya Ngaya Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wamechangisha tofali moja kila kaya na kuanzisha ujenzi wa kituo cha polisi ili kukabiliana na uhalifu ikiwa ni pamoja na uvamizi wakati wa mavuno, serikali ikiahidi kupeleka polisi wa kutosha kitakapokamilika.

Kata ina vijiji sita na kaya 2,324 na wakazi 18,700 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 na mchango wa Mbunge Iddi Kasimu wa Sh. milioni 2.5 ulifanikisha ujenzi wa kituo hicho kutokana na uvamizi kukithiri hususani katika kipindi cha mavuno.

Akizungumza baada ya kutembelea na kukagua ujenzi wa kituo hicho juzi, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Jumanne Sagini, alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Hamisi Katimba, kuhakikisha kituo hicho kinakamilika ili kianze kutoa huduma kwa wananchi.

Aidha, alisema ili kituo hicho kianze kutoa huduma, inatakiwa kukamilisha ofisi za mkuu wa kituo, sehemu ya mapokezi, ofisi ya mashtaka, mahabusu za wanawake, wanaume na vijana na endapo vitakamilika serikali itapeleka askari polisi 16 wa kuanzia ili kudumisha usalama.

"Ngazi ya kata tunatakiwa kujenga vituo vyenye hadhi ya daraja "C" hiki kimekosa vigezo, vituo vingine hakikisheni mnajenga selo za kutenganisha wanawake, vijana na watoto, ofisi ya mashtaka nakuwa na ofisi ya dawati la jinsia la wanawake na watoto," alisema Sagini.

Hata hivyo, alilipongeza jeshi la jadi maarufu kama sungusungu kwa kuendelea kushirikiana na jeshi la polisi katika kupambana na uhalifu usiendelee kujitokeza na kuchafua amani iliyopo, na kuwataka wanapowabaini wahalifu wahakikishe wanatoa taarifa na siyo kujichukulia sheria mkononi.

Mbunge wa Jimbo la Msalala, Iddi Kasimu alisema uwapo wa matukio ya uvamizi wa kutumia silaha baada ya mavuno, ubakaji na wizi ndivyo vilivyosababisha wananchi kuchangishana lengo likiwa kudhibiti vitendo hivyo.

Diwani wa Ngaya-Msalala, Kisusi Ilindiro alisema, mpaka sasa kituo hicho kimeshatumia Sh. milioni 27 kati ya hizo milioni 2.5 zilitolewa na Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Msalala na ili kikamilike kinahitaji Sh. milioni 20 na kuahidi kutekeleza maagizo yaliyotolewa ya ukamilishaji wake.

Mkazi wa kata hiyo, Oswad Richard alisema, ili waweze kupata huduma za kipolisi walilazimika kutembea umbali wa kilometa 15 kwenda na kurudi kituo cha polisi Busangi na Ilogi na kesi nyingi zilikuwa zinaishia njiani bila kupata ufumbuzi na wakati mwingine watuhumiwa kukimbia.



Mafundi wakijenga ofisi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Wilaya ya Musoma Mjini, mkoani Mara jana, utakifanya chama hicho kuondokana na mtindo wa kutumia ofisi za kupanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UWT Shy yadaiwa kuigawa mafungu CCM

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA


BAADHI ya wajumbe wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) Mkoa wa Shinyanga, wamedaiwa kuwa chanzo cha mpasuko wa chama hicho kutokana na kuibuka kwa tabia ya kurekodi sauti za vikao vyao na kuwapelekea baadhi ya viongozi wakiwamo wabunge kwa lengo la kuwachonganisha.

Hayo yamebainishwa juzi na Mwenyekiti UWT Mkoa wa Shinyanga, Grace Bizulu na kuonesha kukerwa na tabia hizo za baadhi ya wajumbe na kusema vitendo hivyo vinakwamisha juhudi za kujenga umoja wao na kusababisha mgawanyiko kwa wabunge pamoja na chama. Aliwaambia wajumbe hao kuwa tabia ya kurekodi sauti wenzao wanapokuwa wakizungumza kwenye vikao, imeanza kusababisha mvurugano katika chama na wabunge hali inayoleta picha mbaya.

"Kama wewe ni miongoni mwa hao wanaopenda kujipendekeza kwa wabunge na kutumia mwanya wa umoja huu acha mara moja, na endapo nikimbaini mtu ambaye bado anaendelea kufanya hivyo, nitamuagiza Katibu asitishe kumuita kwenye vikao vyangu ili tuache kuendekeza majungu," alisema Bizulu.


Aidha, alisema uchaguzi ulishaisha hivyo ni vyema kila mmoja afanye majukumu yake ya kazi ikiwa ni pamoja na kusikiliza na kutatua kero za wananchi na kuzitatua, kwa sababu wote ni watoto wa mama mmoja CCM siyo vyema kugombana.

Naye Mjumbe wa Baraza la UWT Taifa Christina Gule, aliwaomba wanawake wa CCM kuendelea kuwa wamoja na ushirikiano ili waweze kufanya mambo makubwa ndani ya chama na jamii kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kuendelea kutatua kero mbalimbali za wananchi kwa kushirikiana na wabunge wao.



Ukurasa 12

**Ilichofanya halmashauri hii kudhibiti maambukizi mapya**




**Mapya yabainiki vimelea vinavyoishi ndani ya uvimbe wa saratani**

Ukurasa 14

## UJIO VIRUTUBISHO MBADALA

# Mwisho wa 'sumu' kilimo, mifugo vinalinda afya, rutuba ardhini na kufukuza magonjwa

**Elizabeth Zaya na Christina Mwakangale**

WATETEZI wa afya ya binadamu na mazingira wanaonya kuwa kutumia kemikali iwe mbolea za viwandani na dawa dhidi ya viuatilifu na tiba za mifugo ni hatari kwa vile mwisho ni maradhi yasiyoambukiza na vifo.

Aidha, kutegemea zaidi kemikali hizo kunahusishwa na ongezeko la saratani, mashambulizi ya mishipa ya fahamu na hata kutibua nasaba (DNA) za viumbe hai hasa zinapotumika kwa muda mrefu, pia zimechangia kuharibu mazingira na mfumo wa ikolojia.

Ili kuepukana na tatizo hilo, Taasisi ya Afrint Bio Solution kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) inatoa tiba mbadala kwa wakulima na wafugaji kuwekeza pasipo athari kwao na mazingira.



Paluku Emmanuel, akitoa maelezo ya matumizi ya virutubisho kwenye banda la Wizara ya Mifugo na Kilimo katika Maonyesho ya Sabasaba. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

Kwa pamoja wanatoa virutubisho mbadala ambavyo hutumika kiasi kidogo kwa mifugo na kilimo, visivyo na kemikali vinavyostawisha mazao na wanyama kikamilifu.

Dk. Paluku Emmanuel, kutoka Taasisi ya Afrint Bio Solution, anasema virutubisho hivyo vya mifugo hajulikana kama 'Trypi na RojoTic.

Aidha, kwenye kilimo anasema viko vingi kama 'Bio Organic' inayotumika kwenye mboga na matunda. Anataja pia, kupanda majani ya mifugo, maua, alizeti, mpunga pamoja na nafaka nyinginezo na kufukuza wadudu wote waharibifu ikiwamo ndege pamoja na panya.

Ufumbuzi huo unakuja wakati kuna malalamiko ya kukosa uzingatiaji bora wa matumizi sahihi ya dawa kwenye mifugo na kilimo ili kulinda afya na ustawi wa binadamu au walaji .

Lakini pamoja na mimea na mazingira na kwa miaka ya hivi karibuni wafugaji na wakulima wengi wamekuwa wakitumia dawa kwa ajili ya mifugo na kilimo licha ya kudaiwa kuwa zina kemikali.

Aidha, kwa kukosa elimu ya namna ya kutumia dawa hizo au kukosea maelekezo na hata kupuuza walaji wameendelea kupata athari ya kiafya hasa magonjwa yasiyo ambukizwa mfano saratani.

Dk. Emmanuel, anapozungumza na Nipashe kwenye Maonyesho ya Sabasaba, jijini Dar es Salaam, anasema virutubisho hivyo vinanyunyiziwa kwenye mboga na matunda badala ya viautilifu sumu lakini vingine hupandwa kurutubisha ardhi.

"Tukitumia kwenye kilimo hakuna haja ya mbolea kwenye mimea lakini dawa kwenye mifugo. Aidha, hurutubisha ardhi na hata kuongeza uzalishaji." Anasema.

Anasema kadri mkulima anavyotumia virutubisho hivyo ndivyo na ardhi inavyopata rutuba ya kustawisha mazao na kuzidi kuongeza anasema.

Anasema kwa wafugaji, wanapotumia virutubisho hivyo, mifugo inakuwa na afya bila kuugua au kufa ovyo.

Anaeleza kuwa ni mkulima na amevitumia virutubisho hivyo na kupata matokeo mazuri katika baadhi ya mikoa ilipolima ikiwamo Mbeya.

"Katika heka tatu ambazo nilitumia kilo tisa za mbolea ya virutubisho hivyo nilipata magunia 53 ya mpunga. Baada ya kuvuna ilipofika tena wakati wa kulima awamu ya pili, nilirudia kulima tena katika eneo hilo nikavuna magunia 71."

"Mara ya mwisho ni sasa ambako tumevuna magunia 100 katika eneo hilo hilo," anasema Dk. Emmanuel na kuongeza kuwa kwa hiyo inamaanisha mkulima akitumia virutubisho hivi, anaboresha ardhi, anapokuja kuvuna, mazao yake yataendelea kuongezeka."

Kwa hiyo sio lazima mkulima atumie mbolea, hivi virutubisho vinafanya kazi kubwa na bila kuwa na athari kiafya na kuacha ardhi ikiwa na rutuba ya kutosha.

Anasema kadri mkulima anavyozidi kulima kwa virutubisho mara nyingi, ndivyo na ardhi itakavyozidi kurutubika.

Pia, anasema chakula kilicholimwa na virutubisho sokoni kina soko kubwa kuliko kilichozalishwa na mbolea na kemikali za viwandani.

Anatoa wito kwa wakulima na wafugaji, kuhama kutoka kulima au kufuga kwa kutegemea dawa au kemikali badala yake wafanye hivyo bika kemikali hizo.

"Kwa sasa dunia inabadilika, soko kubwa sasa hivi ni kwa vyakula au mifugo inayozalishwa bila kemikali. Tunaamini kwamba si rahisi kufunga viwanda vinavyotengeneza mbolea, lakini tunaweza kupunguza nguvu ya mbolea nyingine, tukatumia zisizo na kemikali na kama unataka kupeleka chakula chako kwenda kuza Ulaya lazima watakuuliza au

Inaendelea Uk. 13

AFYA

# Ilichofanya halmashauri hii kudhibiti maambukizi mapya

Na Jumbe Ismailly, SINGIDA

NDANI ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida kasi ya maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI inapungua, kutokana na juhudi za kuibua watu walioathirika na VVU pamoja na kuwaanzishia dawa za kufubaza virusi kwa wakati.

Mratibu wa Kudhibiti UKIMWI wa halmashauri hiyo, Enea Mwakilembe, anaelezea jinsi elimu inayotolewa ilivyosaidia kuongeza uelewa wa namna virusi vya VVU vinavyosambazwa na njia za kujikinga na maambukizi mapya, kuwakubali pamoja na kuwatunza wanaoishi na ugonjwa (WAVIU).

Kwa mujibu wa Mwakilembe hali ya maambukizi mapya ya VVU imekuwa ikishuka kwa asilimia 1.4 ikilinganishwa na mwaka 2015 ambako yalikuwa asilimia 2.0 wakati kwa mwaka 2022 yameshuka hadi asilimia 0.6.

Anasema kati watu 3,193 waliopima VVU mwaka 2015 waliopatikana na VVU ni 58 sawa na asilimia mbili, wakati mwaka 2016 kati ya 15,031 waliochunguzwa afya waliokutwa na VVU ni 226 sawa na asilimia mbili. Katika mwaka 2917 walibainika kuwa wameambukizwa watu 252, kati ya 17,549 waliopima sawa na asilimia 1.4.

Akitoa takwimu za karibuni anasema mwaka 2021 kati ya watu 37,407 waliopima 341 sawa na asilimia 0.9 walibainika wameambukizwa VVU na kwa mwaka 2022 kati ya watu 41,323 waliopima, 241 sawa na asilimia 0.4 walikuwa na maambukizi ya VVU.

"Hali ya maambukizi imekuwa ikishuka kwani kwa mwaka 2015 ilikuwa asilimia mbili, wakati mwaka 2017 waliopatikana ni asilimia 1.4 na ilishuka hadi asilimia 0.8 mwaka 2020 na kupungua hadi asilimia 0.9 mwaka 2021 na kwa mwaka 2022 ni asilimia 0.6," anasema Mratibu.

Mwakilembe anabainisha kwamba kitengo cha kudhibiti maambukizi ya VVU kinafanya kazi na wadau mbalimbali wakiwamo taasisi ya EGPAF kupitia mradi wa Afya Yangu, SHIDEFA, NACOPHA, mradi wa Hebu Tuyajenge, AMREF na JHPIEGO.

Mratibu huyo anasema huduma wanazotoa ni pamoja na kinga, utoaji elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU pamoja nakufanya tohara bila gharama kwa wanaume ambao wamefikia rika la kubalehe na bado hawajatahariwa kupunguza hatari za kupata na kueneza maambukizo.



Mgonjwa akitumia ARVs dawa za kufubaza VVU. **PICHA: MTANDAO**

Huduma nyingine ni kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya VVU kupitia kampeni mbali mbali kama vile ya upimaji wa saratani ya mlango wa kizazi, upatikanaji na usambazaji vipira ya wanaume katika maeneo mbali mbali kwenye mikusanyiko.

Kupima na kuibua watu wenye maambukizi ya VVU, Mratibu anazitaja juhudi kuwa ni kufanya mikutano ya kutoa elimu, kupima pamoja na kuwachunguza wanaofika hospitalini, vituo vya afya au zahanati wenye viashiria vya VVU.

Anazitaja nyingine kuwa ni kuwatafuta pamoja na kuwapima watu wenye tabia hatarishi katika maeneo wanayopatikana na kuwapima wanawake wanaofanya biashara ya ngono, wanaume wanaofanya ngono kinyume na maumbile, wanaojidunga,wanaotumia dawa za kulevya na madereva wa magari makubwa.

Kadhalika anasema kusambaza vitendanishi na vifaa vinavyohitajika katika masuala ya upimaji kwenye vituo vya kutolea huduma za kwenye jamii, Mratibu Mwakilembe anaongeza kuwa katika tiba na matunzo ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na uhifadhi bora wa kumbukumbu na takwimu za WAVIU.

Kadhalika kusaidia malipo mbali mbali ya vipimo na huduma za msingi za WAVIU, kuongeza nguvu kazi za watumishi kwa maeneo yenye uhaba wa watoa huduma, kusaidia vikundi mbalimbali vya WAVIU kiuchumi na kisaikolojia pamoja na ukusanyaji pamoja na uchambuaji wa takwimu za UKIMWI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Esther Chaula, anafafanua kuwa kutokana na hali halisi iliyopo ya maambukizi ya VVU katika eneo hilo wamejiwekea mipango wa kuhakikisha kiwango cha maambukizi hakiongezeki zaidi ya kupungua siku zote.

Anaitaja mikakati hiyo kuwa ni pamoja na uanzishwaji wa huduma za tiba na matunzo katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya na kuhakikisha dawa za kufubaza VVU na vitendanishi vinapatikana muda wote katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya.

Mikakati mingine, Esther anasema ni kutoa elimu ya maambukizi na faida za matumizi ya dawa za kufubaza VVU, elimu dhidi ya unyanyapaa wa WAVIU na kuhakikisha wapya wote wanaanza dawa mara wagundulikapo.

Mkurugenzi Mtendaji anazitaja njia zinazotumika kuwapata watu wenye maambukizi ya VVU kuwa ni pamoja na kufanya mikutano, kupita katika vijiji mbali mbali kutoa elimu na kupima maambukizi ya VVU, kuwapima nyakati za matukio na sikukuu za serikali kama vile Siku ya UKIMWI Duniani, ya Wanawake na mbio za Mwenge wa Uhuru.

Anayataja makundi ya watu hatarishi ambayo wanayafuatilia kuwa ni pamoja na wanawake wanaofanya biashara ya ngono,wanaoshiriki ngono kinyume cha maumbile, waraibu wa dawa za kulevya pamoja na madereva wa magari makubwa.

## DAMU SALAMA

Akizungumzia kitengo cha damu salama cha halmashauri hiyo, Esther anasema licha ya awali kuwa na kituo kimoja cha St.Carolous Hospitali chenye uwezo wa kutunza na kuongeza damu kwa wagonjwa, kinafanya vizuri na kinajitosheleza kulingana na mahitaji yaliyopo.

Anabainisha pia kuwa kutokana na kuongezeka kwa mahitaji, huduma zinapanuliwa na kwamba wanategemea kuongeza vituo vingine vitatu kwa ajili ya kutunza na kuwaongezea damu wagonjwa katika hospitali ya wilaya na vituo vya afya Mgori na Msange.

Mwenyekiti wa vikundi vya mapambano dhidi ya UKIMWI wilayani Singida, Japheth Nyinginyingi, anasema awali serikali ilikuwa ikiwapatia misaada mbali mbali, ikiwemo chakula na dawa walizokuwa wakitumia kwenye uji kwa ajili ya kuboresha afya zao, vipande vya sabuni, sukari, maharage pamoja na mboga.

Nyinginyingi anaongeza kwamba, imeacha na kwamba kukosekana misaada hiyo iliyokuwa ikisaidia kujitokeza kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU, hadharani, imepungua.

Aidha, imekuwa vigumu kutokana na dhana potofu kwamba wanatumika kwa maslahi ya watu wengine.

Mwenyekiti huyo hata hivyo anasema wakati umefika serikali kwa kushirikiana na wadau kuangalia uwezekano wa kurejesha upya huduma walizokuwa wakipatiwa kundi hilo ili idadi ya wanachama wanaoishi na maambukizi ya VVU iweze kuongezeka na kutoendelea kuogopa kujitokeza hadharani.

Anasema yamekuwapo malalamiko kutoka kwa wanawake wanaoishi na maambukizi ya VVU kukosa wanaume wa kuwaoa baada ya kujitangaza hadharani kuwa wanaishi na maambukizi ya VVU.

Maria Masuda ambaye ni mmoja wa wajumbe wa watu wanaoishi na VVU kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida anabainisha kwamba muungano wa WAVIU katika wilaya hiyo ulianzishwa mwaka 1999 ukiwa na wanachama wasiopungua 12.

Maria anasema tangu kuanzishwa kwa umoja huo wamekuwa wakipata misaada kutoka serikalini, mashirika ya World Vision, AMREF, NACOPHA, EGPAF pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF).

Akifafanua misaada waliyonufaika nayo kuwa ni pamoja na kuwezeshwa kufuga kuku, mbuzi, ng'ombe pamoja na kupatiwa semina za mafunzo ya namna ya kuwahamasisha watu wanaoishi na maambukizi ya virusi vya UKIMWI ili waweze kujitokeza na kutambulika kwa jamii ili wasiweze kujamiiana nao kwa hofu ya kuongeza idadi ya WAVIU hao.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya wilaya ya Singida, Dk.Grace Charles, anasema katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2022 idadi ya watu walioandikishwa kwenye kitengo cha tiba na matunzo imefikia 1,267.

Aidha, anasema katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2022 halmashauri haijapokea fedha kwa ajili ya kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira magumu ambao pia wanaweza kuumizwa na VVU na UKIMWI.

Anawakaribisha wadau mbalimbali ili kuweza kuwasaidia watoto hao, na kwamba halmashauri ina watoto 5,473 walioopo kwenye mazingira magumu na hakuna kituo cha kulelea watoto hao.

MAZINGIRA

# Wanavijiji wengi wanafahamu kuwakabili wanyamapori wakali

**Na Christina Haule, MOROGORO**

MASHAMBULIZI ya wanyamapori kwa raia wanaoishi vijiji jirani na rasilimali hiyo ni tatizo linalojitokeza zaidi miaka ya hivi karibuni.

Kushambulia husababisha vifo, majeruhi, ulemavu na uharibifu wa mazao na makazi ya wanavijiji.

Katika kulinda watu, mazingira, wanyama na mazao, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) inawapa elimu ya kujiepusha na madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu wanavijiji 224 wa wilaya 32 kote nchini kutoka Oktoba 2020 hadi Oktoba 2021.

Mkuu wa dawati la ujirani mwema TAWA, Twaha Twaibu, anasema hayo kwenye mahojiano na Nipashe, akieleza kuwa mafunzo hayo, yametolewa kupitia mikutano 227 iliyofanyika kwenye vijiji vinavyozunguka hifadhi za mapori ya akiba.

Twaibu anasema elimu wanayoitoa ni umuhimu wa uhifadhi wa wanyamapori, mazingira, shoroba na mtawanyiko wa wanyama hifadhini. Aidha, umuhimu wa mpango wa matumizi bora ya ardhi, tabia za wanyamapori wakali na waharibifu mfano tembo, viboko na mamba,

mbinu zinazotumika na jamii kuepuka madhara ya wanyamapori wakali na waharibifu kwa kutumia nyuki, pilipili, mitaro na vitu vinavyotoa sauti kali.

Aidha Twaibu, anasema watumishi wahifadhi kutoka vituo 39 vya mapori ya akiba na kanda wamekuwa wakifanya doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu wanaoingia kwenye maeneo ya vijiji ili kuimarisha usalama wa maisha ya watu dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu.




Kibonzo kinachotoa ujumbe wa jinsi ya kuwakabili wanyama pori akilengwa tembo. **PICHA: TAWA**

Anawataka wananchi majirani na maeneo ya wanyamapori kujiepusha na tabia ya kuwapiga hasa wakali kwa kutumia silaha mbalimbali za kimila au jadi wanapoingia kwenye maeneo yao badala yake watoe taarifa za matukio ya uvamizi huo kwa viongozi ili hatua zichukuliwe haraka.

TAWA kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI) inakamata wanyamapori wakali na waharibifu na kuwahamisha kutoka kwenye sehemu nyingine salama.

Halikadhalika, wanyamapori wakali wamekuwa wakiuawa kama hatua ya mwisho kwa ajili ya usalama wa wananchi kwa mujibu wa Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2019, anasema.

Anaishauri jamii kuacha tabia ya kujenga makazi karibu na hifadhi za mbuga za wanyamapori ili kujiepusha na hatari zikiamo vifo kutokana na wanyama kama tembo, nyati, mamba na kiboko.

Ofisa Wanyamapori TAWA, Joseph Mnyai, anasema zipo faida nyingi zinazopatikana kupitia uwindaji wa kitalii pamoja na utalii wa kama fedha zinazopatikana kuchangia shughuli za kimaendeleo kwa wananchi wanaishi kando ya mapori ya akiba, tengefu na maeneo ya ardhioevu.

Aidha, anasema serikali imeandaa na kuanza kutekeleza mpango wa kitaifa wa kusimamia utatuzi wa migongano baina ya watu na wanyamapori ambao unatekelezwa na taasisi mbalimbali ikiwamo TAWA.

Anasema malengo mkakati katika kutekeza mkakati wa kitaifa wa kuhakikisha wanyama wakali na waharibifu hawaleti shida kwa jamii ni pamoja na kujenga uwezo wa jamii katika kutumia njia mbalimbali za kutatua matatizo yanayoibuka, kuimarisha udhibiti wa wanyamapori wakali na waribifu pamoja na

kusimamia maeneo yanayotenganisha shughuli za kibinadamu na uhifadhi wa wanyamapori.

Anataja malengo mengine kuwa ni pamoja na jamii kufaidika na rasilimali ya wanyamapori, kutoa elimu ya uhifadhi kwa umma, ufuatilia mwenendo wa migongano na kufanya utafiti.

Katika mahojiano na mmoja wa wanakijiji waliopata elimu hiyo, Majuto Juma anaishukuru TAWA kwa kuwapatia mafunzo ambayo watayatumia ili kujilinda na wanyama wakali na waharibifu.

Anasema awali walikuwa wakikumbana na changamoto ya kuvamiwa na wanyama wakali na waharibifu ambao huharibu na kupoteza mazao kama vile mahindi na migomba huku pia miundombinu mbalimbali ikiharibiwa baada ya wanyama wakubwa kama vile tembo na nyati kuvamia vijiji na mashamba yao.

Akizungumzia suala hilo Kamishna wa Uhifadhi TAWA Mabula Misungwi, anawataka wanavijiji vinavyozunguka mapori ya akiba kote nchini kuzingatia elimu wanayopewa na wahifadhi juu ya kujilinda na wanyama wakali na waharibifu.

Misungwi anasema suala la kujilinda na wanyama wakali na waharibifu lisipozingatiwa vyema na wananchi, ni wazi kwamba migogoro baina ya wanavijiji na mapori ya akiba haitakwisha.

Anasema jitihada zinazofanywa na TAWA na serikali zinapaswa kuzaa matunda kwa kuhakikisha wanyama wakali na waharibifu hawaleti madhara yoyote kwa wanadamu na mali zao iwe za mashambani hata za majumbani.

Halikadhalika anaikemea tabia ya jamii nyingi kudharau maagizo, elimu na matamko wanayopewa na TAWA kuhusu kujilinda na wanyama wakali na waharibifu kwa sababu kufanya hivyo ni kujaribu kujisababishia hatari mbalimbali ikiwamo kupoteza maisha kwa kupata madhara kutoka kwa wanyama wakali. Misungwi anakumbusha kuwa TAWA iliyoanzishwa kwa ajili ya kusimamia majukumu ya kiutendaji yaliyokuwa yakisimamiwa na Idara ya Wanyamapori, ina majukumu ya kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali ya wanyamapori na utalii kwenye mapori ya akiba, tengefu na maeneo mengine nje ya TANAPA na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA).

Aidha, inahusika na kuratibu uanzishwaji na usimamizi wa mashamba na bustani za wanyamapori, anasema Misungwi.

# MWISHO WA 'SUMU' KILIMO, MIFUGO VINALINDA AFYA, RUTUBA ARDHINI NA KUFUKUZA MAGONJWA

Inatoka Uk. 11

kutaka uwape cheti cha 'organic' kwa hiyo kama huna unakwama," anasema Dk. Emmanuel.

Akizungumzia virutubisho hivyo, Mtafiti wa TALIRI, Valentino Urassa, anasema kutokuzingatia matumizi bora ya dawa hususani muda wa dawa kukaa ndani ya mwili wa mnyama na kutoka kunachangia jamii kula vyakula vyenye mabaki yake na kuleta usugu wa matumizi dawa hizo kwa binadamu.

"Kwa hiyo mwarobaini pekee ni kuachana na dawa za kemikali na kutumia virutubisho lishe," anasema Urassa.

"Imefika wakati kwa wakulima na wafugaji kubadili mfumo wa kuzalisha vyakula ambavyo havina dawa ili kuepuka madhara ambayo huonekana baadaye.

Kwenye ufugaji kwa kutumia virutubisho hivyo, anasema hukuza mifugo kwa haraka na kuilinda dhidi ya maradhi.

Anasema miongoni mwa faida kutumia kiasi kidogo cha chakula tofauti na wale wasiotumia virutubisho hivyo ambao hutumia dawa.

"Mfano kwa kutumia virutubisho, kuku 500 wanatumia kilo moja kwa mwezi, kwa hiyo haigharimu fedha nyingi kuwalisha. Na katika kuwapatia chakula tunatumia gramu, kwa mfano kama unawapatia lita 40 utatwalisha gramu 40 kwa hiyo inakuwa rahisi. Na wakitumia namna hiyo mpaka saa tano au sita inatosha."

"Kilo moja ya virutubisho inauzwa Shilingi 85,000 na inatumika kwa mwezi mmoja na ukitumia hiyo hutumii tena mpaka wanakuja kuuzwa."

Urassa anasema wametumia maonyesho ya SabaSaba jijini Dar es Salaam(DITF), kutoa elimu hiyo na kwamba mwitikio umekuwa mzuri na wamepokea idadi kubwa ya wanaohitaji kufuga na kulima bila kutumia madawa au kemikali ambayo baadae huleta athari kwa binadamu.

"Niwahamasishe Watanzania kwamba unaweza kufuga au kulima bila hata kutumia dawa ya aina yoyote na ukazalisha vizuri. Na kwa mfano kuku wanaofugwa bila kutumia dawa huwa hawana harufu na unaweza kufugia nyumbani bila kupata usumbufu wa harufu," anasema.

Anasema mifugo inayofugwa kwa kutumia virutubisho haiugui ovyo na magonjwa, kadhalika mazao nayo ni salama zaidi.

AFYA

# Mapya yabainiki vimelea vinavyoishi ndani ya uvimbe wa saratani

## •Ni kulinda, kuleta usugu na kusambaza




Mgonjwa akichunguzwa saratani ya matiti. **PICHA: MTANDAO WA SAYANSI**

**Na Mwandishi Wetu**

MIILI ya wanadamu inatajwa kuwa ni makazi ya aina tofauti ya vijidudu, mfano utumbo, mdomo, pua na ngozi ni nyumbani kwa jumuiya mbalimbali za vimelea ambavyo vinaweza kuwa ni vyema au vibaya kwa afya za watu.

Katika tafiti za miaka ya karibuni wanasayansi wamegundua makazi mengine ya zaidi wanapoishi vimelea au bakteria kuwa ni kwenye uvimbe.

Ni jambo la kawaida kuuchukulia uvimbe kama mkusanyiko wa seli nyingi za mgonjwa ambazo hazifanyi kazi kikamilifu ambazo hazifanyikazi kikamilifu na hukua bila kudhibitiwa.

Aidha, uvimbe ni muungano wa aina tofauti za seli, ambazo zinaashiria kwa kiasi kikubwa ugumu wa kuzishambulia kwa tiba na hata zikiguswa kunakuwapo na uharibifu wa tishu zenye afya.

Lakini uvimbe pia huhifadhi mkusanyiko wa seli kutoka kwa aina nyingine za viumbe hai, bakteria na fungasi.

Baadhi hustawi katika mazingira yanayozunguka uvimbe, huku vimelea au bakteria wengine wakiishi ndani ya seli za saratani zenyewe.

Lakini, hadi hivi karibuni haikubainika wazi vijidudu huwa na jukumu gani ndani ya uvimbe.

Sasa wanasayansi wanaanza kubaini ikiwa vijidudu hivi vinahusika katika ukuzaji wa seli za saratani au ni vijidudu tu vilivyonaswa kwenye uvimbe.

Majibu yanaweza kutoa mbinu mpya za kutibu na kuzuia saratani.

**HULINDA UVIMBE**

Katika utafiti wa mwaka 2017 wataalamu wanagundua kuwa baadhi ya bakteria wanaoishi ndani ya saratani ya kongosho wanaweza kulinda uvimbe kwa kuzima nguvu ya dawa ya chemotherapy inayotumiwa kutibu saratani.

Chemotherapy ni aina ya matibabu ya saratani ambayo hutumia dawa kadhaa kwa nia ya kuponya au kurefusha kiasi maisha au kuondoa dalili zinazojitokeza za maradhi hayo.

Ravid Straussman, mwanabiolojia wa saratani katika Taasisi ya Sayansi ya Weizmann huko Rehovot, Israel, na timu yake wanabaini kuwa aina fulani ya bakteria, inayojulikana kama 'Gammaproteobacteria,' inaweza kuvunja 'gemcitabine', dawa inayotumiwa kutibu aina mbalimbali za saratani, ikiwa ni pamoja na zile zinazopatikana kwenye kibofu cha mkojo, matiti na kongosho.

Inaeleza kuwa bakteria hao husaidia uvimbe huo wa saratani kuwa sugu kwa dawa. Wakati watafiti walipowaingiza bakteria hao kwenye panya wenye saratani ya utumbo, uvimbe wao ukawa sugu kwa dawa hiyo.

Lakini watafiti walipowapa panya dawa ya antibiotiki pamoja na 'chemotherapy', usugu huo ulitoweka.

Utafiti huo unatoa kidokezo cha kuvutia kwa kile kinachoendelea ndani ya uvimbe. Straussman na timu yake sasa wanatarajia kuendeleza utafiti huo kwa kufanya majaribio ya kimatibabu yanayohusisha wagonjwa wa saratani ya kongosho ambao matibabu yao ya kwanza hayakufaulu.

Watawapa wagonjwa 'antibiotic' inayofanya kazi dhidi ya Gammaproteobacteria, pamoja na gemcitabine, ili kuona kama dawa hiyo inaboresha matokeo yao.

**KUITUNZA SARATANI**

Wanagundua kuwa zipo bakteria zinazofanya saratani kuwa mbaya zaidi kwa kuchukua nafasi nyingine katika saratani badala ya kulinda uvimbe dhidi ya dawa ya matibabu. Mwaka 2020, kundi la Straussman lilichambua zaidi ya vivimbe 1,500 za binadamu katika aina saba tofauti za saratani za matiti, mapafu, ovari, kongosho, melanoma, mifupa na ubongo.

Wanagundua kwamba aina zote za uvimbe zilivamiwa na bakteria, ambao waliishi ndani ya seli za saratani na baadhi ya seli za kinga. Aina tofauti za uvimbe zilikuwa na jamii tofauti za bakteria.

"Kila bakteria hizi imezoea mazingira ya kipekee ambayo inaishi ndani yake ," anasema Straussman na kuongeza kuwa katika saratani ya mapafu, walionyesha jinsi watu wanaovuta sigara wana bakteria nyingi ambazo zinaweza kuvunja nikotini, ambayo ni zao au michakato inayotokana na moshi.

Katika uvimbe wa mifupa, tunaona bakteria ambao hubadilisha hydroxyproline, ambayo ni metabolite iliyoboreshwa katika uvimbe wa mfupa."

Hata hivyo bado haijabainika ikiwa bakteria humsaidia mgonjwa kudhibiti seli za saratani lakini zinazopatikana katika aina fulani za saratani ya matiti, kwa mfano, zinaweza kuondoa sumu ya 'arsenate', aina ya uvimbe inayojulikana kuongeza hatari ya saratani ya matiti.

Anasema kuna ushahidi kwamba, katika halinyingine, bakteria wanaoishi kwenye uvimbe wanaweza kufanya saratani kuwa mbaya zaidi na kwamba upo utafiti zaidi unaonyesha jinsi bakteria wanaweza kuwa sehemu ya saratani.

Bakteria pia wanaweza kubadilisha uwezo wa mfumo wa kinga kushambulia na kuharibu seli za saratani, anaongeza. "Kwa kweli tunafanya uchunguzi zaidi mengi zaidi yanahitajika kufanywa ili kufahamu athari za bakteria ndani ya uvimbe wakati wa ugonjwa huu.

**KUCHOCHEA UGONJWA**

Baadhi ya vidokezo kutoka kwenye utafiti wa 2020 uliofanywa na wanasayansi wa China vinaonyesha kuwa baadhi ya bakteria kwenye uvimbe wa matiti wanaweza kurahisisha seli za saratani kuenea katika sehemu nyingine za mwili.

Watafiti wanagundua bakteria wanaoishi ndani ya seli za uvimbe wa matiti zinazozunguka kwenye damu ya panya hutengana na uvimbe wa msingi na zinaweza kusafiri hadi sehemu nyingine za mwili na kukua, hata hivyo, chembe chembe za uvimbe zinapozunguka kwenye mkondo wa damu zinakabiliwa na hali ngumu ambayo hufanya baadhi kupasuka.

Aidha, bakteria nyingi zinazohusishwa na saratani ya utumbo zinaweza kufanya kazi pamoja ili kudhoofisha hali ya mgonjwa.

Wakati wanasayansi walipoondoa bakteria hizi kutoka kwenye uvimbe ndani ya mwili wa panya, vidonda vilionekana kupoteza uwezo wa kukua, ingawa saratani ya matiti ya msingi iliendelea kuongezeka."Kuna ushahidi kwamba vijidudu maalum kwenye utumbo, ngozi na viungo vingine vya utando wa mucous vinaweza kukuza ukuaji na kuendelea kwa uvimbe au kwa njia nyingine kuupinga," anasema Douglas Hanahan, kutoka Taasisi ya Uswizi ya Utafiti wa Saratani ya Majaribio Lausanne, Uswisi.

"Picha ni ngumu sana. Ingawa kuna dalili, hakuna ufafanuzi wa uhakika juu ya nani anafanya nini."

**BAKTERIA WANAOHAMA**

Tafiti zingine zilichunguza bakteria ya mdomo inayoitwa 'Fusobacterium nucleatum', ambayo inahusishwa na ugonjwa wa fizi lakini pia inaweza kuhusika na aina mbalimbali za saratani.

Kuna uwezekano wa bakteria hizi kuhama kutoka kinywa na kugeuka seli za saratani ya colorectal kupitia mkondo wa damu. Kila bakteria hubeba chembe maalum ambazo zinaweza kugeuka na kuwa seli za saratani na kujikuza ndani ya uvimbe.

Baada ya kuanzishwa, bakteria wanaweza kuongeza kasi ya ukuaji na kuenea kwa uvimbe kwa kudhoofisha uwezo wa mfumo wa kinga kuua seli za saratani. Bakteria pia hutumia silaha ya molekuli ambayo hufanya seli za saratani kuwa sugu zaidi kwa tibu ya chemotherapy.

**BBC-SWAHILI**



## VODACOM yatoa tuzo washirika, watoa huduma

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMPUNI ya Mawasiliano na Teknolojia Vodacom Tanzania imetoa tuzo kwa washirika na watoa huduma wake kwa kuzingatia viwango vya usalama mahali pa kazi.

Akizungumza wakati wa kukabidhi vyeti na tuzo hizo jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Vodacom Tanzania Plc, Jaji mstaafu Thomas Mihayo, alifafanua umuhimu wa kuainisha ajenda ya usalama na afya kwenye mazingira ya kufanyia kazi huku akisema kila mmoja ana mchango mkubwa kwenye mafanikio ya Vodacom.

"Kujitoa kwenu, kuzingatia taaluma na kutuunga mkono kwa uthabiti katika kusimamia nguzo hizi kumepelekea mafanikio haya. Kwa kuongezea, milango yetu ipo wazi kupokea maoni, mapendekezo na kushirikiana kwenye jitihada za kujenga mustakabali imara na endelevu zaidi kwa siku za usoni," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Philip Besiimire, alisema kuwa: "Kama kampuni inayojiendesha kiteknolojia, tunazingatia kwa kiasi kikubwa umuhimu wa ubunifu wa kidigitali katika kuboresha shughuli za kiafya na usalama kazini, tukizifanya sehemu za kufanyia kazi kuwa salama zaidi, na kupunguza hatari ya ajali na majeruhi."

Alisema ubunifu wa aina hiyo ni muhimu kwenye kuchangia kupunguza hatari na ajali kwa washirika na watoa huduma wao.

Alibainisha kuwa Vodacom Tanzania inatambua mchango wa watoa huduma wake ambao wanapitia mazingira tofauti ya hatari mara kwa mara kuhakikisha ufanisi wa uendesheaji wa huduma za mtandao na tuzo hizo zinatoa fursa ya kuwapongeza kwa kuwa kiungo muhimu katika kuhakikisha usalama.

"Kwa miaka mingi, Vodacom imekuwa kinara kwenye kutambua umuhimu wa viwango vya ubora katika mnyororo wa utoaji huduma zake na kupelekea kufanikinisha kuwa na miaka 11 mfululizo ya bila ya vifo mahala pa kazi," alisema.

# RC ataka watumishi wazembe wachukuliwe hatua

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, (pichani) ameagiza hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa watumishi waliobainika kufanya uzembe, ubadhirifu wa fedha za umma na kusababisha hoja za ukaguzi zisizo na majibu.

Akizungumza katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino juzi, Senyamule alionya tabia ya baadhi ya watumishi kutotimiza majukumu na wajibu wao wa msingi kwa makusudi na kusababisha hoja za ukaguzi zisizokuwa na majibu.

"Kila mmoja atimize wajibu wake, hoja nyingi hapa zinatokana na uzembe wa baadhi ya watumishi kutotimiza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, wanashindwa kuambatisha nyaraka za msingi zinazohitajika hali inayopelekea kukithiri wa hoja za ukaguzi," alisema Senyamule.

Alisema ili halmashauri hiyo iondokane na hoja nyingi ni lazima Kamati ya Fedha ikutane kila mwezi na kuwa na agenda ya kudumu ya kujadili mwenendo wa namna ya kujibu hoja za mkaguzi wa ndani na zile za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kuchukua hatua stahiki pale inapobainika uzembe wa aina yoyote.



Alitoa rai kwa madiwani kuhakikisha kuwa fedha zinapelekwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kuzingatia mgawanyo wa asilimia 40 na asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa mujibu wa sheria.

Alimwagiza Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Dk. Semistatus Mashimba, mapato ya serikali yanakusanywa kikamilifu na kudhibiti upotevu.

Awali, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya CAG kwa mwaka wa fedha 2021/22 kwenye halmashauri hiyo, Mkaguzi Mkuu wa Nje, Chambi Ngelela, alisema halmashauri hiyo ilipata hati inayoridhisha na ilikuwa na hoja 61 kati hizo 13 zimefungwa na kusalia 48 ambazo utekelezaji wake unaendelea.



Wakazi wa Mtaa wa Mwongozo, Kata ya Nkulabi, jijini Dodoma, wakiwa wamebeba kuni kwa ajili ya kuuza kwa wateja wao jana, ambapo fungu moja la kuni linauzwa kwa bei ya 350/-. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Vijana wenye ulemavu watakiwa kuanzisha vikundi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu mkoa wa Dodoma (Shivyawata), Omar Lubuva, amewaagiza vijana wenye ulemavu kuacha tabia ya kukaa vijiweni na kusubiri wafadhili na kuwataka wajiunge kwenye vikundi ili kupata fursa ya mikopo.

Lubuva aliyasema hayo jana jijini hapo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye mafunzo ya uhamasishaji jamii juu ya masuala ya elimu jumuishi na ukusanyaji wa taarifa za matukio ya unyanyasaji na ukatili dhidi ya wenye ulemavu iliyofanyika Kata ya Nkulabi. Alisema bado kuna dhana potofu miongoni mwa vijana wa kiume na kike ya kukaa vijiweni na nyumbani wakiwa na malengo ya kusubiri ufadhili hali inayowaongezea umaskini.

Aliwataka vijana hao kuungana kwa pamoja ili wapate mikopo inayotolewa na taasisi mbalimbali za kifedha na kuanzisha miradi ya kiuchumi. "Ninawaomba vijana wote wa kike na kiume wenye ulemavu undeni umoja wenu wa vikundi na mbuni miradi yenye tija ambayo itakayowawezesha kupata mikopo inayotolewa na taasisi za kifedha, badala ya kukaa kusubiri misaada kutoka kwa wadau mbalimbali," alisema.

Hata hivyo, alikemea tabia ya baadhi ya vijana wanaokopa fedha hizo na kuzielekeza kwenye matumizi yasiyofaa.

"Mikopo hiyo inayotolewa ikumbukwe kuwa ina malengo ya kuwabeba kutoka ngazi ya umaskini hadi hatua ya kukua kiuchumi, hivyo niwaombe vijana wa kike na kiume kujiwekea malengo zaidi kupitia mikopo hiyo," alisema.

Aidha, aliwahimiza watakapopata mikopo hiyo warejeshe kwa wakati badala ya kusubiri kutaifishiwa kwa mali zao na kupelekwa kwenye vyombo vya kisheria.





# Shule zageuzwa vijiwe kwa kukosekana uzio

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KUKOSEKANA kwa uzio katika Shule za Msingi Madaraka na Maanga, Kata ya Maanga jijini Mbeya, kumesababisha baadhi ya madarasa kugeuzwa kuwa kijiwe cha vibaka kuvutia bangi na kutekeleza uhalifu mwingine.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Hilda Mponzi aliyasema hayo juzi wakati Taasisi ya Tulia Trust inayomilikiwa na Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini ilipokuwa inakabidhi mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa shuleni hapo.

Alisema vibaka wamekuwa wakiingia kirahisi shuleni hapo hasa muda ambao wanafunzi wanakuwa hawapo na kuanza kuvuta bangi na kutumia dawa zingine za kulevya jambo ambalo linahatarisha usalama wa watoto.

"Siku za nyuma walikuwapo hata wale wa kujidunga dawa za kulevya, walikuwa wanakuja hapa, lakini tunawashukuru viongozi wa serikali za mitaa, tulishirikiana na hili likaisha tunaamini uzio utaimarisha zaidi usalama," alisema Mwalimu Hilda.

Pia alisema miundombinu ya shule hizo imekuwa ikiharibiwa na wahuni hao hasa kupasua vioo vya madarasa na hivyo kuifanya shule kuwa na mazingira mabovu.

Aliishukuru Taasisi ya Tulia Trust kwa kuwasaidia saruji hiyo kuwa itasaidia kuongeza kasi ya ujenzi wa uzio unaoendelea shuleni hapo.

Aliomba wadau wengine kuendelea kuisaidia shule kwa kuwa majengo yake yana hali mbaya kutokana na uchakavu.

Diwani wa Kata ya Maanga, Newton Mwatujobhe, alisema shule hizo zilikuwa zinakabiliwa na matatizo mengi ambayo kupitia vikao vya Kamati ya Maendeleo ya Kata walikubaliana kuanza kutatua moja baada ya lingine.

Alisema awali waliwahi kujenga uzio kwa kutumia matofali ya kuchoma, lakini baadhi ya watoto watundu kwa kushirikiana na vibaka waliubomoa na kuwalazimu kuanza ujenzi kwa kutumia matofali ya saruji.

Alisema walianza kujenga kwa kuchangishana na kuomba misaada kutoka kwa wadau na ndipo Dk. Tulia akaahidi kuwapatia mifuko 50 ya saruji.

"Tulianza kuomba miundombinu ya shule zetu zote kuboreshwa lakini wadau walipokuja kukagua walipendekeza tuanze na Shule ya Msingi Maanga ambayo sasa imekamilika na iko katika hali nzuri," alisema Mwatujobhe.

Kadhalika, kwenye ukarabati wa shule hiyo walipokea Sh. milioni 180 kutoka serikali kuu ambazo ndizo zilizotumika kukarabati shule hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya Dk. Tulia Ackson, Ofisa Habari wa Taasisi ya Tulia Trust, Joshua Mwakanolo, alisema kiongozi huyo aliamua kutoa msaada huo baada ya kuona wananchi wa kata hiyo wakijitolea kujenga uzio huo.

Alisema alitoa maelekezo kwao kwenda kupeleka saruji hiyo ili kuharakisha mradi huo na wanafunzi wasome katika mazingira mazuri na rafiki kwao.

Aliwaomba wananchi wa eneo hilo kuendelea kumuunga mkono Dk. Tulia kwenye shughuli zake kwa maelezo kuwa ana moyo wa kujitolea kwa ajili ya maendeleo yao wenyewe.

Shule za Msingi Madaraka na Maanga ni miongoni mwa zinazokabiliwa na matatizo mengi ikiwamo vyumba vya madarasa na vyoo.

## Mbunge afanya ziara kukagua miradi ya jimbo

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

MBUNGE wa Jimbo la Lupa wilayani Chunya Mkoa wa Mbeya, Masache Kasaka, ameanza ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi katika jimbo hilo pamoja na kusikiliza kero za wananchi.

Masache alianza ziara hizo juzi kwa kukutana na makundi mbalimbali ya wananchi wa wilaya hiyo kwa ajili ya kusikiliza maoni yao kuhusu namna ya kuzitekeleza ziara hizo.

Alifanya mazungumzo na watumishi wa Halmashauri ya Chunya na baadaye akazungumza na umoja wa wazee wa wilaya hiyo.

Masache alisema watumishi wa halmashauri hiyo wanafanya kazi vizuri na kwa ushirikiano jambo ambalo linafanya maendeleo kwenda kasi zaidi.

"Nawashukuru kwa kazi kubwa ambayo mnayoifanya, muda wote hata nikiwa bungeni huwa nafuatilia kinachoendelea huku ili nijuwe na mimi nifanye kipi, sasa nimekuja nataka kufanya ziara kwenye vijiji ili nijuwe matatizo yanayowakabili wananchi," alisema Masache.

Alisema serikali inatoa ushirikiano mkubwa anapoomba miradi ya maendeleo na mpaka sasa serikali inaendelea na uboreshaji wa miundombinu.

Alisema inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali wilayani humo ikiwamo miundombinu ya barabara, maji, vituo vya kutolea huduma za afya na miundombinu ya elimu.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Tanzania, Prof. William Pallangyo (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Kimataifa wa Baraza la Wahitimu Chuo Kikuu Mzumbe, Dk. Lucy Massoi, kuhusu uchangiaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa kike ndaki ya Mbeya, alipotembelea banda la chuo hicho kwenye Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# H'shauri kutumia zao la kakao kujenga shule za vipaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI za wilaya tatu za Mkoa wa Mbeya zinazozalisha kakao mkoani hapa, zimeanza mikakati maalumu ya kutumia mapato yanayotokana na zao hilo kujenga shule za wasichana za vipaji maalumu ili kuinua kiwango cha elimu.

Shule hizo ambazo zitajengwa katika Halmashauri za Kyela, Rungwe na Busokelo, zitakuwa za bweni ili ziwe sehemu ya suluhisho la matatizo yanayoikabili kundi hilo hasa kubakwa, kusababishiwa ujauzito na utoro.

Mikakati hiyo ilipangwa juzi kwenye kikao kilichoitishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera na kuwashirikisha wadau mbalimbali wa zao hilo kutoka katika halmashauri zote tatu ambazo ndizo zinaongoza kwa uzalishaji wa kakao nchini.

Wadau walioshiriki ni pamoja na kampuni za ununuzi wa kakao, wasambazaji wa magunia ya kufungashia zao hilo, chama kikuu cha wakulima pamoja na wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa wilaya hizo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera alisema shule hizo zitajengwa katika halmashauri hizo kwa kuanzia halmashauri ya Kyela ambayo ndiyo inayoongoza ikifuatiwa na Busokelo na watamalizia katika Halmashauri ya Rungwe.

Alisema baada ya shule hizo kukamilika wataanza kuzijengea mabweni ili wanafunzi wasiishi mitaani na badala yake waishi kwenye mabweni hayo.

"Hizi shule zitaitwa Cocoa Girls na ya Kyela, tunataka ianze mwezi Januari 2024, kwahiyo tunawaomba wadau watoe ushirikiano ili tufanikishe jambo hili mapema," alisema Homera.

Alisema halmashauri ndizo zitakuwa zinazisimamia shule hizo kuanzia kwenye ujenzi mpaka kwenye uendeshaji ili ziwe na mafanikio.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Ernest Hinju, alisema mkoa huo una shule nyingi, lakini umeamua kuongeza kasi ya ujenzi kutokana na taarifa ya Sensa ya Watu na Makazi kuonyesha kuwa kuna ongezeko kubwa la watu katika mkoa huo.

Alisema utaratibu huo wa kushirikiana na wadau wa mazao mbalimbali mkoani humo kujenga shule uliasisiwa na Mkuu wa Mkoa Homera alipofika mkoani humo kwa kuanza kuwahamasisha.

Alisema walianzia katika Wilaya ya Chunya kwa kujenga shule katika Kata ya Lupatingatinga ambayo walianza kujenga kwa ushirikiano kati ya halmashauri na wadau wa kilimo cha tumbaku na baadaye wakafuata Shule ya Pareto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

"Kwa hiyo huu utaratibu ni mzuri na tunamshukuru sana Mkuu wa mkoa kwa ubunifu wake, sasa tuwaombe wazazi na walezi watupe ushirikiano kwa kupeleka watoto wao kwenye hizi shule ili hii dhamira itimie," alisema Mwalimu Hinju.

Alisema ujenzi wa miundombinu hiyo utasaidia kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa mkoa huo ikilinganishwa na mikoa mingine.

Mmoja wa wadau wa kilimo kakao, Richard Temu ambaye ni mwakilishi wa Export Trading Company, alisema kwenye makubaliano yao waligawana kila mdau kujenga majengo yake kulingana na ramani watakazopewa.

Alisema ujenzi huo utaanza Julai 15 mwaka huu na watajenga madarasa mawili huku akisisitiza kuwa shule hiyo itakuwa ni alama kubwa kwao.

Wadau mkoani Mbeya kwa muda mrefu walikuwa wanajadili namna ya kuweka alama katika maeneo hayo ambayo walikuwa wanavutana kujenga kati ya shule ama vituo vya afya mpaka Mkuu wa mkoa, alipowashauri kujenga shule.

# CUF: Hatuna mgogoro na chama chochote cha siasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Hamad Masoud amesema chama hicho hakina mgogoro na chama chochote cha siasa licha ya kutofautiana kisera na vyama vingine.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar wakati wa uzinduzi wa timu ya uhamasishaji wa chama hicho uliopewa jina la turufu kuelekea uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Alisema tofauti hizo zisifanye kuigawa Zanzibar wala Tanzania na ni vyema wanasiasa wakayapa kipaumbele maridhiano ya kisiasa ili kupata maendeleo. "CUF tupo vizuri hatutaki migogoro wala kukaribisha migogoro maridhiano tumeyaweka mbele," alisema Masoud.

Alisema licha ya misukosuko iliyopitia chama hicho, kwa sasa kipo imara na uchaguzi ujao wa mwaka 2025 wanachukua madaraka ya kuongoza nchi na kuendeleza maridhiano ya serikali ya umoja wa kitaifa.

"Endapo juhudi zetu za kushika dola hazijatosha japo umakamu wa kwanza wa rais uje CUF, ili tuendeleze GNU ambayo CUF ndiyo waasisi wa maridhiano hayo," alisema.

Akizungumzia Muungano, Hamad alisema wanataka wa haki na wenye kuheshimika ili kila upande uridhike na kunufaika kwa mujibu wa hali ilivyo.

Alimpongeza Rais Dk. Mwinyi, kwa kuondoa dhambi ya watu kupigwa ovyo, ikilinganishwa na zamani.

Alisema hata kesi za kisiasa zimeondoka ikilinganishwa na miaka ya nyuma na kwamba kulikuwa na kesi nyingi za kisiasa za kubambikiziana.

Kadhalika, licha ya kufanikiwa Zanzibar inakabiliwa na changamoto ya njaa watu kuwa na maisha magumu.

Hata hivyo, alipongeza kwa hatua za uwekezaji zinazochukuliwa na serikali, kuendelea kutumia hekima na busara ili nchi isiingie katika machafuko. Said Omar, Mwenyekiti wa Wilaya ya Mjini wa chama hicho alisema, chama kinahitaji umoja ushirikiano, mshikamano na utulivu.

"Lazima kurejesha hadhi ya chama hicho, bila ya umoja, mshikamo, utulivu na amani kwa sababu chama hicho hakitasonga mbele," alisema.

Mwenyekiti wa turufu wa chama hicho, Atie Magram, alisema lengo la kuanzisha kikundi hicho ni kufanya ushawishi wa wanawake kushiriki katika harakati za kisiasa ili kuleta usawa wa kijinsia na kuongeza hamasa na ari ya chama.



Wakazi wa Unguja wakisoma vipeperushi vyenye ujumbe mbalimbali vya Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Watu Duniani yaliyofanyika kitaifa, Tunguu mjini Zanzibar juzi.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wawili washikiliwa kwa wizi wa sola za barabarani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, linawashikilia watu wawili kwa kosa la wizi wa betri zinazotumika katika sola za taa za barabarani mali ya serikali. Akizungumza jana na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Richard Mchovu, alisema Julai 10, mwaka huu majira ya saa 1.30 usiku eneo la Migombani, ilikamatwa gari yenye namba za usajili Z.707 DF aina ya Suzuki Carry na kukutwa likiwa limepakia betri.

Alisema betri zilizokamatwa ni nne aina ya allgrand zinazotumika katika sola za barabarani ambazo ni mali ya Serikali ya Zanzibar. Aliwataja watuhumiwa waliohusika na wizi huo kuwa ni Omar Abeid Embedodo (22), mkaazi wa Kisauni na Eradius Karoli Katoto (26), mkaazi wa Mahonda na baada ya kuhojiwa walikiri kuiba betri hizo na nyingine nne ambazo waliuza kwa Sh. 120,000.

Alisema katika gari hilo wamekutwa na sururu ambayo inatumika kuchimba barabara wakati wakitekeleza uhalifu huo. Aidha, alisema Jeshi la Polisi linaendelea kuzuia uhalifu katika maeneo ya mkoa huo kwa kushirikiana na wananchi kupitia vikundi shirikishi na wananchi kuendelea kudumisha vikundi hivyo ili kuleta tija maeneo yao.

Alisema polisi imewakamata wahalifu wa matukio mbalimbali ikiwamo wizi, uporaji, unyang'anyi na utapeli na uchunguzi utakapokamilika watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

# Serikali yachukizwa wanaume kusuka nywele

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema kuwa haipendezwi na haiungi mkono tabia ya baadhi ya wanaume kusuka nywele kwa sababu ni kinyume cha maadili, silka na utamaduni wa Mzazibari.

Waziri wa Utalii, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu taarifa zilizosambaa katika vyombo vya habari ikiwamo mitandao ya kijamii kuhusu hukumu ya faini ya milioni moja kwa mwanaume anayesuka nywele.

Alisema suala la wanaume kusuka kiutamaduni na kisilka halikubaliki na kwamba serikali itaendelea kutoa elimu ya madhara ya wanaume kusuka.

Alisema utaratibu wa kumtambua mgeni mwanamume aliyeingia nchini ambaye amesuka zipo na serikali inaendelea kuheshimu haki za binadamu.

Waziri alisema mbinu wanayotumia ni kutoa elimu kwa jamii ili kutokomeza vitendo vya uvunjifu wa maadili ikiwamo ya wanaume kusuka.

"Hili la wanaume kusuka tukisema tuachie haya ndiyo mambo yanayoleta vitu vya hatari hasa kwa vijana wetu kwa hivyo mbinu kubwa tutakayoitumia ni kutoa uelewa na elimu kuhusu hili kwamba haistahiki mwanamume kusuka," alisema.

Aidha, alisema serikali itaendelea kuheshimu utamaduni wa watu wengine na wanapokuja wageni wakiwa wamesuka hawatawazuiwa kuingia nchini kwa sababu utaratibu huo uko wanakotoka.

Kwa wasanii wa Zanzibar, alisema suala la wanaume kusuka halikubaliki na kusema kwamba wanaume kutosuka utalii unaporomoka siyo kweli.

Alisema yapo mataifa makubwa likiwamo la Marekani kuwapo wasanii wanaoimba wakiwa wamejisitiri na kuvaa vizuri na kwamba mambo ya kuyakuza kwamba ili msanii aonekane mzuri lazima asuke ni vyema kuheshimu utamaduni, silka na desturi.

Hata hivyo, alisema Sheria ya Utamaduni ya Zanzibar namba saba ya mwaka 2015 pia ni kosa kwa Wazanzibari kuchora tatuu kwa njia zote.

Viongozi wa dini wamegongelea msumari marufuku ya wanaume kusuka nywele au kuvaa mapambo ya kike, baada ya Shekhe Khamis Shaban Khamis, kusema ni haramu katika dini ya Kiislamu mwanamume kusuka kwa sababu anajifananisha na yule ambaye anastahiki kusuka nywele ambaye ni mwanamke.

Alisema kusuka nywele kwa wanamume ni katazo lenye hukumu na dini imetoa maelekezo kuwa ina haki ya kufuata hukumu iliyowekwa na serikali ni sahihi kwa hukumu iliyowekwa ya kifungo cha miezi sita jela au faini ya Shilingi milioni 100.

Askofu wa kanisa la RGC Charles Kiyengo, alisema mwanamume kusuka inaendana na utamaduni mfano za Kiimasai ambazo zinaruhusu jambo hilo, lakini siyo kwa tamaduni za kizanzibari. Aidha, alisema kama mtu tamaduni yake inakataza mwanamume kusuka ni busara kutosuka kama ilivyo kinyume na utamaduni wa Mtanzania kwamba hairuhusu mapenzi ya jinsia moja.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KIWANJA KINAUZWA

**KIWANJA KIPO KISUKURU** SEGEREA **JKT DSM,** KINA UKUBWA WA MITA ZA MRABA **(SQM) 2252,** KIWANJA KIMEPIMWA KINA HATI,
**BEI MILIONI 60.**
KWA MAWASILIANO:
**0754 857523, 0655857523**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SIKUJUA MALOMBA HANKWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili T.379 DKY, yenye Chassis No. NCP600059954, Engine No.2NZ2513896, Engine Capacity 1290 aina ya TOYOTA IST. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya polisi.
**NML/RB/340/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER CHRISTOPHER KHAKI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 487 ALR – LANDROVER PICK-UP.** Chassis namba **167464.** Engine namba **901838288**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**ARU/MON/RB/232501/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA**
**Mkoa TANGA**
**Usimamizi wa mirathi Na. 120/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU................. PRISCUS PATRICK MASSAWE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA .............ELESIA DASTAN NYAMWELA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26 mwezi 07 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 11 mwezi 7 mwaka 2023

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MJINI TANGA

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HAIKA JUMA MSENGI** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba ya usajili **MC 231 CWZ AINA YA TVS**. Chassis namba **MD625AF76M1400682.** Engine namba **AF7AM1800756.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DOD/DOD/RB/345658/2022.**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**LEGENDS AUCTION MART AND GENERAL BROKER LIMITED** Kwa Idhini na Mamlaka tuliyopewa na **MAENDELEO BANK PLC** tunatoa notisi ya **SIKU KUMI NA NNE (14) TU, YA KULIPA DENI UNALODAIWA** kuanzia siku ya tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya mnada wa hadhara wa kuuza DHAMANA ulizoweka kwenye mkopo kama ratiba inavyoonyesha.

| S\N | JINA LA MDAIWA\MDHAMINI | DHAMANA MAHALI ZILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | EAG GROUP LIMITED | 1. COMMERCIAL BUILDING, PLOT NO 1094, BLOCK M, FOREST AREA, MBEYA CITY<br>2. RESIDENTIAL BUILDING PLOT NO 2014, BLOCK M, FOREST AREA MBEYA CITY. | 29\07\2023 Kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea. |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
3. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa.
4. Gharama zote za kubadili hatimiliki ni za mnunuzi
5. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. **0714939933/0713857349**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ASHURA RASHID KYUSA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 406 EAT – TOYOTA HILUX.** Chassis namba **LN1070017138.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi:
**SOG/RB/788/2023.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**JUMA SAIDI MSISI** Anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria (passport) yenye namba **TAE348099** iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**MOR/MOR/RB/233958/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YONA JAKTA MLIGILICHE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 717 BNR – SUZUKI SWIFT.** Chassis namba **HT51S809224.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **SOG/RB/787/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ISSA HASHIM RAMADHANI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipikii yenye namba za usajili MC 226 BCM aina ya BAJAJ BOXER, Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu Taarifa ya polisi;
**DOD/DOD/RB/395226/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA KILOSA**
**KITUO CHA MIKUMI**
**MKOA WA MOROGORO**

**SHAURI LA MADAI/NDOA NO.78/2023**
**JINA LA MDAI: JOYCE ERASTO MAGARI**
**JINA LA MDAIWA: ABDALLA LUPEMBE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za madai katika Mahakama za Mwanzo)**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai) :Fedha ths.210000/=alikopa kwa mdai pesa kwajili ya biashara.
Kwahiyo unatakiwa kuhudhulia binafsi katika mahakama hii tarehe 14 mwezi wa 07 mwaka 2023 sa 2:30 Asubuhi kwa mujibu wa madai hayo vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO:kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri ya Mahakama hii leo tarehe 10 Mwezi 07 mwaka2023.

.........
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MIKUMI

## KUPOTEA KWA CHETI



**Nankondo Semigambo Mvungi,** anatangaza kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Nne (Form Four) chenye Namba ya Mtihani **S.5032-0034** kilichotolewa na Baraza la Taifa la Mitihani kupitia Shule ya Sekondari Uchira Girls Islamic cha Mwaka 2015.
Kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi kilicho karibu, Taarifa ya Polisi **LGW/RB/178/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI NAMBA. 11 YA 2023**
**TWAHA HAMIM BALALI: ............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**YOHANA ANTHONY NTAWA: .........MJIBU MAOMBI**
**LEONARD THADEI SAID:...............MJIBU MAOMBI**
**RICHARD SIMON NYANGE:...............MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**YOHANA ANTHONY NTAWA**
**LEORNAD THADEI SAID**
**RICHARD SIMON NYANGE**

POPOTE MLIPO Mnaarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Morogoro tarehe 20/07/2023 mbele ya Mwenyekiti E.mogasa ninyi wenyewe binafsi au mtume muwakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa baraza leo tarehe 23 mwezi june 2023.

E.MOGASA
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FLORENCE KASSERA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba T 281 AXD. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/URA/B/229649/2023**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Rafiki wa Mugabe azuiwa kugombea urais Zimbabwe

**HARARE, Zimbabwe**

WAZIRI wa zamani wa serikali ya Zimbabwe, Saviour Kasukuwere, ambaye alikuwa rafiki wa kiongozi wa nchi hiyo, Robert Mugabe, amezuiwa kugombea nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika wiki chache zijazo.

Kasukuwere alikuwa na nia ya kugombea nafasi hiyo na kushindana na rais wa sasa Emmerson Mnangagwa.

Jaji wa mahakama kuu ya Harare, alibatilisha ombi la Kasukuwere la kugombea kama mgombea huru wiki chache tu baada ya Tume ya Uchaguzi ya Zimbabwe kukubali karatasi zake za usajili.

Wakili Lovedale Mangwana, akipinga uamuzi wa chombo hicho akisema kuwa Kasukuwere si mpigakura aliyesajiliwa, hivyo hana sifa ya mgombea kutokana na kuishi nje ya Zimbabwe kwa zaidi ya miezi 18.

Kasukuwere ni mfuasi mkuu wa Mugabe ambaye aliwahi kuwa kamishna wa kisiasa wa Zanu-PF na waziri wa vijana na wazawa katika serikali ya rais wa zamani.

Aliikimbia nchi baada ya mapinduzi ya kijeshi yaliyomwingiza Rais Emmerson Mnangagwa madarakani mwaka 2017.

Alirejea kwa muda mfupi mwaka wa 2018, lakini akakimbilia tena Afrika Kusini akihofia mateso ya kisiasa.

**BBC**




Polisi wa Kenya akifyatua bomu la machozi katika kukabiliana na waandamanaji jijini Nairobi jana. **PICHA: AP**

# Polisi, waandamanaji wakabiliana Kenya, mabomu ya machozi, risasi zarindima

**NAIROBI, Kenya**

POLISI nchini Kenya wamekabiliana na waandamanaji walioingia katika barabara ya miji mbalimbali nchini humo kupinga hali ngumu ya maisha.

Katika kukabiliana na waandamanaji hayo, polisi walitumia mabomu ya machozi kuwatawanya, huku wakiwakamata watu kadhaa waliokuwa kwenye maandamano hayo.

Maandamano hayo ya wafuasi wa upinzani yalianza mapema asubuhi, licha ya kupigwa marufuku na polisi.

Mkuu wa jeshi la polisi nchini humo, alisema kuwa mamlaka haina lingine ila kuchukua hatua zinazohitajika kutawanya maandamano hayo aliyoyaita haramu.

Barabara kuu za Nairobi, Kisii, Kisumu na Nyeri zilikuwa tupu na video za mtandaoni zilionyesha barabara zikiwa zimefungwa katika maeneo kadhaa.

Biashara nyingi zimesalia kufungwa na usafiri umesimama.

Ijumaa iliyopita, makabiliano kati ya waandamanaji wa upinzani na polisi yalisababisha vifo vya watu sita katika miji kadhaa.

Wadereva wa magari ya umma katika miji kadhaa wamejiunga na maandamano hayo na kusitisha shughuli zao kupinga kupanda kwa gharama ya mafuta.

Wataalamu wa njia za kidijitali pia nao walijiunga na maandamano, wakielezea wasiwasi wao kuhusu gharama za mafuta, ukosefu wa marekebisho ya bei na masuala ya usalama.

Wanaoandaa maandamano hayo walihimiza ushiriki mkubwa nchini Kenya kote, wakitaka kufutwa kwa sheria mpya ya fedha inayoongeza ushuru wa mafuta maradufu na kuweka ushuru wa nyumba wa asilimia 1.5 kwa wafanyakazi.

Rais wa Kenya, William Ruto, alitetea sheria ya fedha iliyositishwa kwa muda, akisema kuwa itashughulikia masuala ya ulipaji wa madeni na kuunda nafasi za kazi kwa vijana wasio na ajira.

Alishutumu upinzani kwa kuhujumu mustakabali wa mamilioni ya vijana wasio na ajira na kuapa kuzuia kupoteza maisha kutokana na maandamano.

Mahakama kuu jijini Nairobi ilisitisha utekelezwaji wa sheria ya fedha, ikitaja kuna wasiwasi wa kikatiba.

**BBC**

## Korea Kaskazini yajaribu kombora lenye nguvu

**SAOUL, Korea Kusini**

KOREA Kaskazini imerusha kombora lingine linalosadikiwa kuwa la masafa marefu (ICBM), maofisa wa Japan na Korea Kusini wameripoti.

Kombora hilo la masafa marefu lilipaa kwa zaidi ya saa moja kabla ya kutua karibu na maji ya Japan, jana asubuhi.

Urushaji huo umekuja baada ya Korea Kaskazini kutishia kulipiza kisasi dhidi ya kile ilichosema ni uvamizi wa hivi karibuni wa ndege za kijasusi za Marekani katika eneo lake.

Mapema wiki hii nchi hiyo ilitishia kutungua ndege hizo.

Marekani imepuuza shutuma hizo ikisema kuwa doria zake za kijeshi zinazingatia sheria za kimataifa.

Wasiwasi wa usalama umeongezeka katika rasi hiyo mwaka huu baada ya Korea Kaskazini kufanya majaribio ya silaha mpya.

Nchi hiyo pia iliongeza urushaji wa makombora mwaka 2022 ikiwa ni pamoja na yale yenye uwezo wa kufikia ardhi ya Marekani.

Katika kujibu, Marekani na Korea Kusini zimeongeza mazoezi yao ya kijeshi ya pamoja katika peninsula hiyo.

Korea Kaskazini, imeendelea na urushaji wa makombora yake ikifanyia majaribio makombora mapya ya ICBM na mwezi Aprili kombora linalotajwa lenye nguvu zaidi lilirushwa.

**BBC**

## Miili ya watu yakutwa jangwani

**Tunis, Tunisia**

MIILI ya wahamiaji wawili imepatikana kwenye eneo la jangwani karibu na mpaka wa nchi za Tunisia na Algeria, siku kadhaa tangu kuzuka uhasama baina ya wenyeji na wageni katika mji wa mwambao wa Sfax.

Kugundulika kwa miili hiyo ilielezwa na ofisa mmoja wa mahakama na shahidi mwingine aliyekataa kutaja jina lake kwa sababu za usalama.

Kulingana na msemaji wa mahakama ya wilaya ya Tozeur iliyoko kusini mashariki mwa Tunisia, mwili wa kwanza ulipatikana siku 10 zilizopita kwenye jangwa la Hazoua na mwingine ulipatikana Jumatatu ya wiki hii.

Ofisa huyo alisema mamlaka zimefungua uchunguzi wa kifo cha mashaka ili kubaini sababu za watu hao wawili kupoteza maisha.

Wahamiaji kutoka mataifa ya kusini mwa jangwa la Sahara, waliokuwa wakiishi kwenye mji wa Sfax nchini Tunisia wametumbukia kwenye ghasia ziliosababishwa na uhasama na wenyeji baada ya kifo cha mwanaume mmoja raia wa nchi hiyo kilichotokea Julai 3. Mwanaume huyo alidungwa kisu wakati wa makabiliano kati ya pande hizo mbili.

**DW**

HABARI MICHEZO

# TABORA UNITED YAIANGUKIA FIFA

**Na Saada Akida**

SIKU moja baada ya taarifa ya kufungiwa kusajili, uongozi wa klabu ya Tabora United (zamani Kiyatosce FC), umeliandikia barua Shirikisho la Kimataifa la Soka (FIFA) kuomba kupewa muda wa kumlipa aliyekuwa kocha wao, Ahmed El Faramawy Yousef Mostafa Soliman.

Uongozi huo umeandika barua hiyo kupitia Shirikisho la soka nchini (TFF), wakiomba pia kuruhusiwa kufanya usajili.

Tabora United imefungiwa na FIFA kufanya usajili baada ya Soliman kushinda kesi yake ya madai aliyoifungua kuwashtaki Tabora United kwa kumvunjia mkataba kinyume na sheria wakati huo ikiitwa Kiyatosce.

Akizungumza na Nipashe jana, Mratibu wa timu hiyo, Rashid Hassan, alisema wamepokea taarifa hizo za kufungiwa na tayari wameanza juhudi za kulipa.

"Ni kweli Soliman aliwahi kuifundisha Kitayosce kwa sasa tunapambana kuhakikisha tunamlipa fedha zake, lakini tumeomba kwa mamlaka husika kutupa muda wa kulipa lakini waturuhusu kusajili," alisema Hassan.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ofisa Habari wa TFF, Clifford Ndimbo alisema klabu ya Kitayosce FC na Fountain Gate, inayoshiriki Ligi ya Championship zote zimefungiwa kusajili wachezaji.

Alisema uamuzi huo umefanywa na FIFA baada ya kocha Soliman raia wa Misri kushinda kesi za madai dhidi ya klabu hizo.

"Baada ya Soliman kushinda kesi klabu hizo zitakuwa zimemlipa ndani ya siku 45 tangu uamuzi huo ulipotolewa, lakini hazikutekeleza hukumu hizo.

Wakati Fifa imezifungia klabu hizo kufanya uhamisho wa wachezaji wa kimataifa, TFF limezifungia kufanya uhamisho wa ndani," alisema Ndimbo kwenye taarifa hiyo iliyotoka juzi.

Aidha, Ndimbo kwenye taarifa hiyo alisema TFF inazikumbusha klabu kuheshimu mikataba ambayo zinaingia na wachezaji pamoja na makocha ili kuepuka adhabu mbalimbali ikiwemo kufungiwa usajili iwapo klabu inahitaji kuvunja mkataba na mchezaji au kocha inatakuwa kuzingatia sheria za mkataba.



Mkurugenzi wa Masoko wa kampuni ya kubashiri michezo ya M-Bet Tanzania, Allen Mushi, akifafanua jambo jana mbele ya waandishi wa habari wakati wa kumtangaza mshindi wa 'Perfect12'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Buku yampa shabiki Yanga mamilioni ya M-Bet

**Na Mwandishi Wetu**

SHABIKI wa Mabingwa wa Ligi Kuu, Yanga na klabu ya Manchester United ya England, Ezekiel Mwang'onda (34), amesema ndoto yake ya miaka saba katika kubashiri imekuwa kweli baada ya kushinda kitita cha Shilingi 234,272,830 kupitia mchezo wa Perfect12 wa kampuni ya michezo ya kubashiri ya M-Bet Tanzania.

Mwang'onda ambaye ni mjasiriamali ameshinda mamilioni hayo baada ya kubashiri kwa usahihi jumla ya mechi 12 za ligi mbalimbali duniani.

Alisema kuwa amekuwa akibashiri kwa kipindi kirefu bila mafanikio, lakini mara baada ya kujishughulisha na kampuni ya M-Bet, amepata bahati kwa muda mfupi sana.

"Nimekuwa nikibashiri kwa takribani miaka saba sasa, hivi karibuni, nikaamua kubashiri na M-Bet kwa sababu kubwa tatu, sababu ya kwanza ni dau, ambapo unatumia sh1,000 tu kubashiri mechi 12, sababu ya pili idadi ya washindi ambao wamekuwa wakishinda mara kwa mara na tatu, uharaka wa kupata fedha za ushindi na huduma bora kwa washindi.

Sababu hizi tatu zimenifanya kuhamia huku na sasa nimeingia nyumba ya mabingwa ambao pia ni mamilionea," alisema Mwang'onda.

Alisema kuwa pamoja na shughuli nyingi kusimama, M-Bet iliendelea kuweka mikeka ya kubashiri ikishirikisha mechi mbalimbali pamoja na zile za nchi za Amerika ya Kusini.

"Mimi mara nyingi huwa sifuatilii ligi za Amerika ya Kusini, hata hivyo sikuacha kubashiri na kuendelea kufuatilia kuweka dau na M-Bet na kushinda kiasi kikubwa cha fedha. Nina majukumu kibao na fedha hizi nilizoshinda zitasaidia kukuza biashara yangu na kuwekeza katika miradi mingine," alisema Mwang'onda ambaye ni mkazi wa Kyela, mkoani Mbeya.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi, alisema Mwang'onda ameungana na washindi wengine wa droo ya Perfect12 na kuwaomba Watanzania wenye umri zaidi ya miaka 18 kuendelea kubashiri kupitia michezo yao mbalimbali ili kushinda fedha na kubadili maisha.

"Nampongeza Mwang'onda kwa ushindi huu mkubwa na kikubwa zaidi. Nawaomba vijana wenye umri kuanzia miaka 18 kubashiri na M-Bet ili kujaribu bahati yao," alisema Mushi.

## Dk. Kikwete kuwaaga wapanda mlima 61 kampeni ya GGML KiliChallenge-2023

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu Dk. Jakaya Kikwete kesho anatarajiwa kuwaaga washiriki 61 watakaopanda Mlima Kilimanjaro kupitia kampeni ya 'GGML KiliChallenge -2023' inayolenga kukusanya fedha kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi (ATF) na kuendeleza mapambano ya kutokomeza Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Kampeni hiyo ilianzishwa mwaka 2002 na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa ushirikiano na Tume ya Kudhibiti Ukimwi nchini (TACAIDS).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Tixon Nzunda ilisema baada ya Dk. Kikwete kuwaaga washiriki hao katika lango la Machame kesho, watapokewa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu katika lango la Mweka Kibosho Julai 20 mwaka huu saa 3 asubuhi.

Aidha, akifafanua kuhusu kampeni hiyo, Makamu Rais wa AngloGold Ashanti- GGML anayeshughulikia miradi endelevu Ghana na Tanzania, Simon Shayo alisema mwaka huu jumla ya washiriki 35 watapanda mlima huo kwa njia ya kawaida ilihali washiriki 26 wataupanda mlima kwa kutumia baiskeli.

## JKU yachagua Azam Complex Shirikisho Afrika

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAWAKILISHI wa Zanzibar katika michuano ya Kimataifa Kombe la Shirikisho barani Afrika, CAF, timu ya JKU imeuchagua Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi jijini Dar es Salaam kucheza mechi yao ya nyumbani katika michuano hiyo.

JKU imeuchagua uwanja huo kutokana na viwanja vya Gombani, Pemba na Amaan kilichopo Unguja kuwa katika matengenezo ambayo kulingana na kalenda ya CAF michezo hiyo itaanza wakati viwanja hivyo vitakuwa havijakamilika.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa timu hiyo, Shazil Khatib, alisema wameoamba Uwanja wa Chamazi katika michezo yao yote ya nyumbani hata kama watafanikiwa kuvuka hatua ya awali.

Alisema tayari wametuma taarifa zao CAF juu ya maamuzi hayo ya michezo yao kutochezwa Visiwani Zanzibar badala yake watacheza Tanzania bara. "Tayari tumefanya taratibu za kuomba Uwanja wa Chamazi, kuchezwa michezo yetu yote ya Nyumbani katika michuano hii ya Kombe la Shirikisho Afrika, na tayari katika taarifa zetu ambazo zinatakiwa CAF juu ya ushiriki wetu tumetuma Uwanja wa Chamanzi ndio utakuwa Uwanja wetu waa nyumbani," alisema Khatibu.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**POGBA OFA NENE**

KIUNGO wa kati wa Juventus na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 30, atapewa ofa ya pauni milioni 128 kwa miaka mitatu ili kujiunga na klabu moja nchini Saudi Arabia. **(Gazzetta dello Sport)**

**KANE AITAKA BAYERN**

MSHAMBULIAJI wa Tottenham na England, Harry Kane anataka kujiunga na Bayern Munich msimu huu wa joto huku mabingwa hao wa Bundesliga wakifikiria kuwasilisha ofa ya tatu kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. **(ESPN)**

**SCOTT AKARIBIA BOURNEMOUTH**

KLABU ya Bournemouth iko mbele ya Tottenham, West Ham na Wolves katika harakati za kumsaka kiungo wa Bristol City, Alex Scott mwenye umri wa miaka 19. **(Teamtalk)**

**GYOKERES KUONDOKA**

MCHEZAJI Viktor Gyokeres anatazamiwa kuondoka Coventry kwenda Sporting Lisbon katika siku zijazo huku klabu hiyo ikitarajia ada inayoweza kufikia pauni milioni 20.5 kwa ajili ya mshambuliaji huyo wa Sweden mwenye umri wa miaka 25. **(Mail)**

**CHERKI ATAKIWA CHELSEA**

KLABU ya Chelsea inajiandaa kupeleka ofa ya kwanza kwa mshambuliaji wa Lyon, Rayan Cherki mwenye umri wa miaka 19. **(ESPN)**

**ELANGA AIVUTIA EVERTON**

EVERTON inavutiwa na mshambuliaji wa Manchester United na Sweden, Anthony Elanga mwenye umri wa miaka 21. **(Foot Mercato)**

**GUSTAVO ATAKIWA**

KLABU ya Burnley imemfanya kiungo wa kati wa Coventry, Mholanzi mzaliwa wa Brazil, Gustavo Hamer mwenye umri wa miaka 26, kuwa chaguo lao linalofuata. **(Telegraph)**

**ONANA AKARIBIA MAN**

KLABU ya Manchester United inakaribia kufikia makubaliano ya kumnasa mlinda mlango wa Inter Milan na Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 27. **(Sky Sports)**

**FOREST YAMTAKA HENDERSON**

KLABU ya Nottingham Forest ipo kwenye mazungumzo na Manchester United kuhusu mpango wa kumnunua mlinda mlango wa England, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 26, na pia wanafikiria kumnunua kipa wa Wolves Mreno Jose Sa mwenye miaka 30. **(Telegraph)**

**RICE SAFI ARSENAL**

ARSENAL ina matumaini ya kukamilisha usajili wa kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24, kabla ya kikosi hicho kuelekea Marekani kwa ziara yao ya kujiandaa na msimu ujao Jumapili. **(Sky Sports)**

**LARSEN AWANIWA**

KLABU ya Southampton inafikiria kumnunua winga wa Hoffenheim na Denmark, Jacob Bruun Larsen mwenye umri wa miaka 24. **(Mail)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FRED AFIKIRIA MUSTAKABALI NDANI YA MANCHESTER UNITED

Vilabu kadhaa vimeonyesha nia ya kumwania kiungo huyo wa kati wa Brazil...

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Fred anafikiria mustakabali wake pale Old Trafford huku klabu kadhaa zikimwania, 90min imebainisha.

Kiungo huyo wa kati wa Brazil alijiunga na United Juni 2018, lakini akakosa nafasi chini ya kocha wa sasa, Erik ten Hag katika miezi ya mwisho ya msimu uliopita, akianza mechi mbili pekee za Ligi Kuu England chini ya Mholanzi huyo baada ya timu hiyo kufungwa 7-0 na Liverpool Uwanja wa Anfield.

Usajili wa United wa Mason Mount mwezi huu umemsukuma Fred, ambaye kwa sasa ana umri wa miaka 30, kutathmini chaguo lake huku nafasi ya kikosi cha kwanza ikiwa ni ngumu kupatikana katika msimu mpya.

Ten Hag pia angependa kusajili kiungo mwingine kabla ya dirisha la uhamisho kufungwa, huku Sofyan Amrabat wa Fiorentina akitakiwa.

Fred inaonesha wazi hayumo kwenye mipango ya muda mrefu ya United na klabu iko tayari kumruhusu aondoke kwa bei inayofaa wakati wa dirisha hili la uhamisho.

United wana matumaini kwamba wanaweza kurejesha kati ya paumi milioni 20 hadi 25 katika mauzo yoyote yanayoweza kufanyika.

Fulham inavutiwa nae, lakini wanamthamini Fred kwa chini ya pauni milioni 15 - chini kabisa ya hesabu ya sasa ya United.

Mchezaji huyo alionekana akizungumza na kocha wa Fulham, Marco Silva nje ya Old Trafford baada ya mechi ya mwisho ya ligi msimu uliopita, ambapo pande hizo mbili zilikutana.

Fred amebadilisha wakala hivi karibuni na ana chaguzi zingine za kuondoka - huku klabu za Saudi Arabia zikiwa vinawania kumsajili huku vikiendelea kufagia wachezaji wa hadhi ya juu kutoka barani Ulaya.

Mchezaji mwenzake Fred wa zamani wa United, Paul Pogba anavutiwa sana na Al Ahli na Al Ittihad, ambapo N'Golo Kante na Karim Benzema ni miongoni mwa majina makubwa ambayo tayari yamechukua hatua hiyo.

Inafahamika kuwa Roma ya Jose Mourinho ilizungumza na wawakilishi wa Fred - Mourinho alimsajili Fred kule United wakati wa enzi yake kama kocha - ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 bado hajafanya uamuzi wa wapi pa kucheza.

# MESSI ATUA MAREKANI, KUTAMBULISHWA JUMAPILI




**IAMI, Marekani**

LIONEL Messi ametua Ft. Lauderdale Jumanne akijiandaa kwa hafla ya utambulisho itakayofanywa na klabu yake mpya ya Inter Miami CF, Jumapili.

Messi aliwasili akiwa na mkewe na watoto huku klabu pia ikitoa tangazo la kuthibitisha tukio la kukaribishwa, ambalo limeitwa "The Unveil," na litaanza saa 6 mchana Jumapili kwenye Uwanja wa DRV PNK wa timu hiyo.

Mashabiki wenye tiketi za msimu mzima wa Inter Miami wataingia bure.

Katika mahojiano na Televisheni ya Argentina kabla ya kutua Marekani, Messi alisema atajitolea kwa kila kitu kwa ajili ya klabu hiyo ya MLS, ambayo imeweka rekodi ya kucheza mechi 10 mfululizo bila ushindi kufuatia sare ya 2-2 Jumapili dhidi ya D.C. United.

"Mawazo yangu na kichwa changu havitabadilika na nitajaribu, popote ninapopaswa kuwa, kujitolea kwa uwezo wangu mwenyewe na klabu yangu mpya, kuendelea kucheza kwa kiwango cha juu," alisema Messi akikiambia kipindi cha TV cha Argentina cha Llave a la eternidad.

Akizungumzia familia yake kuhamia Marekani, aliongeza: "Tunafurahia uamuzi tuliofanya. Tumejiandaa na tuna hamu ya kukabiliana na changamoto mpya, mabadiliko mapya."

Inter Miami bado haijafanya rasmi usajili huo, baada ya kufikia makubaliano na gwiji huyo wa Argentina, ambaye alikaa kwa misimu miwili na mabingwa wa Ligue 1, Paris Saint-Germain baada ya kuondoka Barcelona.

Miami inalenga mechi yake ya Julai 21 ya Kombe la Ligi dhidi ya Cruz Azul ili Messi acheze mechi yake ya kwanza kwa klabu hiyo.

Messi atakuwa tena na kocha wake wa zamani wa Argentina na Barcelona, Tata Martino, ambaye alichukua nafasi ya kuinoa timu hiyo mwishoni mwa Juni.

Messi mwenye umri wa miaka 35, ameshinda kila tuzo kuu inayopatikana kwake wakati wa uchezaji na kuwa miongoni mwa wachezaji bora zaidi wa wakati wote.

Pamoja na kutunukiwa tuzo ya Ballon d'Or kama mchezaji bora wa dunia mara saba, Messi ameshinda mataji 43, mataji 35 kati ya hayo aliyabeba akiwa Barcelona ambayo ni mataji 10 ya LaLiga, nane ya Supercopa, saba ya Copa del Reys na mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Messi aliondoka katika klabu hiyo ya Katalunya msimu wa joto wa 2021 kama mfungaji bora wa klabu akiwa na mabao 672.

Huku Barcelona ikiwa kwenye matatizo ya kifedha, Messi alilazimika kuondoka na kukaa PSG misimu miwili iliyopita, ambapo alishinda mataji ya Ligue 1 miaka yote miwili.

# Caicedo hataikataa Chelsea

**LONDON, England**

KIUNGO wa kati wa Brighton, Moises Caicedo amekiri kuwa hataweza kukataa kuhamia Chelsea msimu huu wa joto.

Caicedo ndiye anayelengwa zaidi na The Blues ili kujaza safu yake ya kiungo baada ya kuondoka kwa Mason Mount, Mateo Kovacic, N'Golo Kante na Ruben Loftus-Cheek, na kwa muda mrefu wamekuwa kwenye mazungumzo na Brighton kuhusu kumsajili msimu huu wa joto.

Kinachobaki ni bei ya Brighton ya pauni milioni 100 ambayo ni ya chini kuliko ile ya uhamisho wa Declan Rice kwenda Arsenal.

Kiungo huyo wa kati wa West Ham amegharimu ada ya pauni milioni 105 na Brighton hawaamini kwamba, Caicedo anatakiwa kuwa nafuu zaidi.

Mazungumzo kati ya klabu hizo mbili yameonekana kuwa magumu, lakini Chelsea ilionekana kutokumbana na matatizo kama hayo katika mazungumzo na Caicedo, ambaye alikubali kuwa hataweza kuwakataa The Blues msimu huu wa joto.

"Ni timu kubwa..., hiyo ni kweli," alisema Caicedo akimwambia mwandishi, Maria Jose Flores alipoulizwa kuhusu nia ya Chelsea. "Timu ya kihistoria na siwezi kusema hapana, kwa sababu ni timu kubwa, ya kihistoria na nzuri.

"Mji pia ni mzuri. Una kila kitu kizuri."

Brighton wameonyesha nia ya kuona Chelsea wakitoa ofa kwa beki wa kati Levi Colwill kama sehemu ya biashara hiyo ya kumnunua Caicedo, lakini The Blues wameweka wazi kuwa hawakubaliani na wazo kama hilo.

Colwill aling'ara msimu uliopita akiwa kwa mkopo Brighton na wanataka kumbakiza huki, Liverpool na Manchester City zikimwania pia.

Colwill anatarajiwa kuripoti kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya akiwa na Chelsea katika siku zijazo na atazungumza na kocha, Mauricio Pochettino kuhusu hatma yake katika klabu hiyo, baada ya kuzungumza waziwazi wakati wa majira ya joto kuhusu nia yake ya kuona anacheza kikosi cha kwanza.

"Lazima nicheze mwisho wa siku," aliwaambia wanahabari baada ya msimu wake wa ushindi wa Ulaya akiwa na timu ya taifa ya Vijana ya England chini ya umri wa miaka 21.

Chelsea ina wachezaji kadhaa wa kati kwenye rada zao msimu huu wa joto lakini kwa sasa wanaelekeza nguvu zao kwa Caicedo.

# Man City yakataa kumuuza Alvarez

**MANCHESTER, England**

MAOFISA wa Manchester City wamecheka uvumi kwamba, wanaweza kuwa tayari kuachana na mshambuliaji, Julian Alvarez msimu huu wa joto, kwa mujibu wa 90min.

Bayern Munich wameonyesha nia ya kutaka kumsajili Alvarez, ambaye alikuwa na kibarua kizito cha kumsaidia Erling Haaland kwenye Uwanja wa Etihad msimu uliopita.

Alvarez mwenye umri wa miaka 23, ambaye anaonekana kuwa mmoja wa washambuliaji bora chipukizi wa mchezo huo, alifunga mabao 17 katika mechi 49 katika msimu wake wa kwanza pale Manchester na sasa ametajwa kuwindwa na klabu kadhaa Ulaya.

Hata hivyo, vyanzo vimethibitisha kwa 90min kwamba City wamefurahishwa na mchango wa Alvarez na hawana mpango wa kumpoteza msimu huu wa joto, huku mshindi huyo wa Kombe la Dunia pia anafahamika kuwa na furaha katika klabu hiyo.

Hisia za Alvarez kuhusu hali yake ndani ya City ziliwekwa wazi Machi, aliposaini mkataba mpya wa miaka mitano na bado kuna nia ya kuendelea kufanya kazi pamoja pale Etihad.

Bayern Munich wamefahamishwa vyema kwamba hakuna nafasi ya kumsajili Alvarez msimu huu wa joto.



**HABARI MICHEZO**

# AZAM FC YAANZA KUCHEZA ZA KIRAFIKI

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Azam FC kesho kinatarajia kucheza mechi yake ya kwanza ya kirafiki tangu itue Tunisia kwa ajili ya kambi ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano.

Azam imepanga kucheza mechi nne za kirafiki na kesho itaanza kwa kucheza na dhidhi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan.

Azam itakipiga na timu hiyo ambayo msimu uliopita ilitinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuitoa Yanga, lakini baada ya hapo inatarajiwa kucheza mechi zingine tatu dhidi ya timu za CS Sfaxien, US Monastir na Esperance zote za Tunisia.

Akizungumza na Nipashe toka kwenye Jiji la Sousse nchini humo, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hasheem Ibwe alisema kupata mechi za kirafiki na timu zinazocheza mechi za kimataifa ndiyo ilikuwa dhamira yao kwenda kuweka kambi nchini humo.

"Tunategemea siku ya Ijumaa (kesho) kucheza mchezo wa kwanza wa kujipima nguvu na hii ni dhamira tulioiweka tangu tuko Dar es Salaam kwamba tutacheza mechi za kirafiki za hadhi ya klabu ambazo huenda tukakutana nazo kwenye michuano ya kimataifa lakini zitatuweka vizuri kujiandaa na timu za nyumbani, tunatarajia kuanza kucheza na Al Hilal Omdurman ya Sudan baada ya hapo kuna michezo mingine mitatu utacheza, mechi hizi zitatoa nafasi kwa benchi letu la ufundi kuangalia nini cha kufanya," alisema Ibwe.

Akizungumzia kambi, alisema inakwenda vyema na tayari shughuli iliyokuwa inakusudiwa na Kocha Msenegal, Youssouph Dabo, imeshaanza na amekuwa akitoa dozi kwa wachezaji wake ili kutegeneza kikosi imara.

"Kikosi kiko kwenye hali nzuri, walipofika walifanya mazoezi ya kutoa uchovu baada ya safari ndefu, lakini ile shughuli pevu imeshaanza ya kujiandaa na msimu mpya kila mchezaji ameonyesha utayari, kujituma na kuonyesha kuwa anastahili kuwa kwenye sehemu ya kikosi cha mwalimu na hata mwenyewe ameridhishwa na kile kinachofanywa na wachezaji wake na ameanza kutoa dozi kwa ajili ya kukifanya kikosi kiwe imara," alisisitiza.

Alilisifu eneo na hoteli waliyofikia kuwa ni sehemu nzuri yenye utulivu lakini hoteli ina kila kitu kinachohitajika na wachezaji hawalazimiki kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa ajili ya mazoezi.



Kiungo wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto' akiwa katika mazoezi ya kwanza ya timu hiyo Mjini Sousse nchini Tunisia juzi. **PICHA: BINZUBERY**

# Mashujaa FC yaanza kushusha vifaa

**Na Adam Fungamwango**

SIKU moja tu baada ya kumtangaza Mohamed Abdallah 'Bares' kuwa Kocha Mkuu, klabu ya Mashujaa FC imeanza kufanya usajili kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu baada ya kuwachukua washambuliaji Adam Adam kutoka Ihefu na Abdulnasir Asaa Mohamed 'Gamal' kutoka Mlandege ya Zanzibar.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana inasema kuwa imewasajili wachezaji hao kwa ajili ya kuboresha kikosi cha timu hiyo iliyopanda daraja hivi karibuni.

Kocha Bares aliiambia Nipashe jana kuwa wachezaji hao watasaidia timu hiyo kwa kuwa anawafahamu.

Bares alikuwa kocha wa Gamal wakati wote wakiwa Mlandege kabla ya kocha huyo kuja Tanzania bara.

Wakati wa kutambulishwa, Bares aliahidi kufanya usajili mzuri utakaowatoa Mashujaa FC hapo ilipo na kuipeleka mbele, ikiwa ni mara ya kwanza katika historia ya timu hiyo kupanda Ligi Kuu.

"Tutafanya usajili mzuri na wa kuvutia, ila ikumbukwe wachezaji ni wale wale tu, ni kiasi cha kutoka kule na kumleta hapa, kinachohitajika atengenezwe na yeye mwenyewe ajitume awe msaada kwenye timu," alisema kocha huyo.

Aliema anataka kuiboresha timu hiyo ili kuweza kutoa upinzani kwa timu nyingine za ligi kuu.

## Simba kushtua nchi usajili

INATOKA UK. 24

faida kubwa kwa mashabiki wao kwa kuweka kadi maalum zikiwamo za watoto ambazo zitasimamiwa na wazazi wao.

Katika mkutano wa utambulisho wa ushurikiano huo, wachezaji wa Simba, Jean Baleke na mchezaji wao mpya Che Fondoh Malone walikuwapo na kupata fursa ya kuwasalimia mashabiki.

Katika salamu zake, Malone ameahidi kushirikiana na wachezaji wenzake aliowakuta klabuni hapo kuipa mafanikio.

Alisema Simba ni timu kubwa hivyo anaamini yupo sehemu sahihi itakayomsaidia kufikia malengo yake kama mchezaji.

## Yanga kukipiga na Kaizer Chiefs

INATOKA UK. 24

huyo anaamini atakuwa na mchango mkubwa ndani ya kikosi chake.

"Ni mchezaji mzuri, klabu imemfuatilia kwa muda na naamini ana jambo la kuongeza kwenye klabu yetu," alisema Gamondi.

Alisema kila mchezaji atapata nafasi ya kumwona kwenye mazoezi ambayo yameanza jana.

"Nimeanza kazi, kila mchezaji nitamuona mazoezini, lakini niseme tu nimeridhishwa na wachezaji wapya, tutaandaa timu ambayo itatutoa Yanga ilipofikia msimu uliopita na kusogea mbele zaidi," alisema Gamondi.

Ofisa habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe alisema wamemsajili beki huyo ambapo uongozi unaamini wamepata mchezaji mzuri atakayekwenda kuleta ushindani kwa wenzake waliopo ili kuwafanya nao kutobweteka.

"Tumemsajili mmoja wa wachezaji wazuri kutoka Uganda, kacheza msimu mmoja tu SC Villa akitokea timu ya daraja la kwanza, lakini msimu mmoja tu alichaguliwa kuna mmoja wachezaji bora wa msimu, pia kuwa nahodha wa kikosi hicho halafu moja kwa moja anaitwa kwenye kikosi cha timu ya taifa, Uganda Cranes panga pangua amecheza kwenye mechi za CHAN, kusema kweli klabu yetu inajivunia kumpata," alisema Kamwe.

Alisema usajili huo siyo wa kwenda kuziba nafasi ya mtu, bali ni kuleta ushindani kwa waliopo kwa sababu wanaamini kuwa bado wana kikosi bora ambacho kimefanya makubwa msimu uliopita.

"Sisi tunasajili wachezaji ambao wataleta changamoto tu kutoka pale ambapo tulikuwa msimu uliopita, kupandisha ubora wetu kuelekea msimu unaofuatia, kama tulifanya vizuri kwenye michuano mbalimbali iliyopita lazima tutengeneze nafasi za ushindani kwenye kikosi, mfano nafasi ya ulinzi basi mchezaji aone kuna wengine ambao wataleta ushindani unaona kwenye idara yetu kuna Dickson Job, Bakari Mwamnyeto, Ibrahim Abdallah 'Bacca', sasa ameongezeka Gift upinzani utaongezeka zaidi," alisema Kamwe.

Wakati huo huo klabu hiyo imemtangaza kocha msaidizi mpya raia wa Senegal, Moussa Ndao kuchukua nafasi ya Cedric Kaze ambaye mkataba wake umemalizika.

# Michezo

Alhamisi Julai 13, 2023
Nipashe





## Messi atua Marekani, kutambulishwa J'pili

UKURASA 22




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu ya Simba, Salim Abdallah 'Tyr Again' (kulia), Mtendaji Mkuu wa CRDB, Abulmajid Nsekela (wa nne kushoto), wakiwa pamoja wachezaji na viongozi wengine wa klabu hiyo baada ya kutia saini makubaliano ya ushirikiano jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# SIMBA KUSHTUA NCHI USAJILI UNAOKUJA

●●● Uongozi waweka wazi wanajiandaa kutambulisha mchezaji anayetoka kwenye klabu kubwa Afrika...

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Simba umesema hivi karibuni watatikisa nchi kwa kutamtambulisha mchezaji mkubwa kutoka katika klabu kubwa Afrika baada ya kukamilisha usajili wake.

Kauli hiyo imetolewa jana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa klabu hiyo, Salim Abdallah 'Try Again', katika uzinduzi wa ushirikiano baina ya klabu hiyo na Benki wa CRDB.

Try Again alisema kama watu walioamini tayari wamemaliza usajili wamekosea kwa sababu bado hawajamaliza na kwa sasa wanajiandaa kumtangaza mchezaji mpya ambaye ataleta gumzo nchini katika kipindi hiki cha usajili.

"Mchezaji huyu anayekuja nchi itasimama, ni mchezaji mkubwa anayekuja kuitikisha nchi, wana Simba wasubiri waone kwa sababu tumeamua kufanya maboresho makubwa kwenye kikosi chetu," alisema Try Again.

Aidha, alisema baada ya mchezaji huyo na wengine watatu watakaokuja kutambulishwa, watasafirishwa kwenda Uturuki kuungana na kikosi cha timu hiyo ambacho kimeweka kambi nchini humo.

Try Again alisema usajili unaofanyika sasa unachangiwa pia na Rais wa heshima wa klabu hiyo, Mohamed Dewji ambaye amedhamiria kurejesha heshima ya klabu hiyo.

**MAKUBALIANO NA BENKI**

Simba imeingia ushirikiano na Benki ya CRDB ambapo wanachama wa klabu hiyo watapata kadi maalum za wanachama zitakazotambulika na benki hiyo.

Kwa kufungua akaunti yake maalum pamoja wanachama na mashabiki kutambulika rasmi kupitia benki hiyo na kujiandikisha kwa kufungua akaunti.

Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Abdulmajid Nsekela alisema ushirikiano huo utanufaisha pande zote na wanachama wa klabu hiyo watapata fursa ya kupata huduma mbalimbali kutoka CRDB.

"Nimefurahi ushirikiano huu na niweke wazi kuwa Simba ni klabu ya kwanza hapa nchini kumiliki akaunti yake maalum, lakini kuwapa kipaumbele mashabiki na wapenzi wa klabu hiyo, kwa mashabiki wanawake watapata fursa ya kufungua akaunti maalum ya Simba Queens ambayo itakuwa na faida nyingi kwao," alisema Nsekela.

Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema ushirikiano huo utakuwa na

UKURASA. 23

## Yanga kukipiga na Kaizer Chiefs 'Mwananchi Day'

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, akisema ameridhishwa na usajili wa beki wa kati Gift Fred, uongozi wa timu hiyo umetangaza kuileta nchini klabu ya Kaizer Chief watakayocheza nayo kwenye kilele cha tamasha la Siku ya Wananchi.

Kilele cha Siku ya Mwananchi imepangwa kufanyika Julai 22 ambapo Yanga watatumia kutambulisha wachezaji wake tayari kwa ajili ya msimu mpya wa mashindano.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana jioni na mechi ya kimataifa ya kirafiki itachezwa saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa na Yanga itakuwa ikicheza kwa mara ya kwanza na timu hiyo ya Afrika Kusini.

Katika hatua nyingine, kocha Gamondi amesema ameridhishwa na usajili wa beki mpya Fred.

Gamond alisema kwa wasifu wa beki

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >